epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Aprili 3, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581635
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**ANCELOTTI: MADRID WANA FAIDA ZAIDI YA MAN CITY**




# Vikundi WhatsApp vyaagizwa kujisajili

UKURASA 3



**Majaliwa:** Bangi mpya imewateka miaka 13 hadi 24 UKURASA 2

**Mabasi** ya mwendokasi sasa majiji yote nchini UK.9



**TRA** yakusanya Trilioni 6.63/- robo ya tatu 2023/24 UKURASA 4

**Samia** atia saini sheria uchaguzi na tume huru UK.8



Msajili wa Jumuiya za Kiraia katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Emmanuel Kihampa. **PICHA: MTANDAO**

## Ole Sendeka afunguka kiini cha risasi 18

UKURASA 9




## Polisi Zanzibar: Hakuna marufuku kutokula mchana

UKURASA 17

**MICHEZO** **PACOME AMPA MZUKA GAMONDI SAUZI** UK.24 **KATUNI** UK.6




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akiwasha Mwenge wa Uhuru, wakati wa uzinduzi wa Mwenge huo, katika viwanja vya Chuo cha Ushirika Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: OWM**

# Majaliwa: Bangi mpya imewateka vijana wenye miaka 13 hadi 24

**Na Waandishi Wetu,** MOSHI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema viriba tumbo na uzito uliozidi, vinaelekea kuwa janga la taifa, huku asilimia 42 ya wanawake walio katika umri wa kuzaa, wakikabiliwa na upungufu wa damu.

Pia amesema aina mpya ya bangi yenye kiasi kikubwa cha kilevi, kinachofahamika kama 'cha Arusha' na skanka, vimegundulika kuwa na sumu nyingi ambayo huchanganywa kwenye sigara na watu wakishaitumia wanabadilika na kuwa vichaa.

Akizungumza jana katika uzinduzi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa uliofanyika Viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), mjini hapa, Majaliwa alisema vijana waliogundulika kuathiriwa na sumu hiyo ni wenye umri wa miaka 13 hadi 24.

Kuhusu janga la kitaifa linalosababishwa na viriba tumbo na uzito uliozidi, Waziri Mkuu alisema: "Tunayo asilimia 42 ya wanawake walio katika umri wa kuzaa wanaokabiliwa na changamoto ya upungufu wa damu.

"Tatizo la uzito uliozidi na kiriba tumbo linaelekea kuwa janga la kitaifa, lakini pia linakuwa ni kisababishi kikubwa cha magonjwa yasiyoambukiza kama vile kisukari, saratani na magonjwa ya moyo."

Aliitaja mikoa 12 inayoongoza kwa udumavu wa watoto chini ya miaka mitano na ambao wamekosa lishe bora, hivyo kukabiliwa na udumavu kwa zaidi ya wastani wa kitaifa ni Iringa, Njombe, Rukwa, Geita,Ruvuma, Kagera,Simiyu,Tabora, Katavi,Manyara, Songwe na Mbeya.

Majaliwa alisema kumeibuka aina nyingine ya bangi, yenye kiasi kikubwa cha kilevi kinachofahamika kama cha Arusha na skanka. Alisema aina hiyo ya bangi yenye sumu nyingi, huchanganywa kwenye sigara, lakini watumiaji wake wakishaitumia wanabadilika na kuwa vichaa.

"Ni wakati mzuri sasa hasa vijana ambao mmekuwa mkitumika na kutumia hiki cha Arusha na skanka, muache ili kunusuru maisha yenu. Cha Arusha na Skanka itawapoteza kwenye mwelekeo; na mtalifanya taifa hili likakosa Watanzania.

"Jambo la kusikitisha ni kwamba vijana wamekuwa wakitumia na wanafahamu hiki kitu cha Arusha na Skanka na idadi kubwa ya waathirika au waraibu wa bangi ni watoto, vijana wenye umri wa miaka 13 hadi 24.

"Mikoa inayolima bangi nchini kwa wingi ni Mara, Morogoro, Arusha, Pwani, Kagera na Mwanza. Nitoe onyo kwa wakulima kuacha mara moja, hatua kali zitachukuliwa kwa wanaojihusisha na kilimo hicho haramu," alisema

Waziri Mkuu pia aliwasisitiza wananchi kujitokeza kwa wingi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitongoji na Vijiji wa Mwaka 2024, kugombea nafasi mbalimbali na katika mikutano ya kampeni.

Pia alishauri wananchi kuchagua viongozi waadilifu, wazalendo na wachapakazi ili washirikiane nao katika kuleta maendeleo.

Mwenge huo wa Uhuru utakimbizwa katika mikoa 31 nchini kwa siku 195 kwenye wilaya 195.

**Imeandikwa na Godfrey Mushi na Mary Mosha**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
01.04.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **04.04.2024** mnatangaziwa hadi **18.04.2024** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Bandari ya Dar Es Salaam** kuelekea **Mzenga,** gari hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB54202 na DS00TG GP / NRB53910**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita 28.5** |
| **Upana** | - | **Mita 5.50** |
| **Kimo** | - | **Mita 4.80** |

3. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar Es Salaam** hadi **Mzenga** kupitia Barabara ya **Mandela,** Barabara ya Morogoro gari litasafiri muda wa mchana ***( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117902602


## Zaidi ya wananchi 1,000 kuondolewa kupisha maboresho uwanja wa ndege

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

Serikali inatarajia kuwaondoa zaidi ya wananchi 1,000 waliovamia eneo la Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ili kuendelea na hatua za kukiboresha ili kikidhi vigezo vya kimataifa.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nyamagana (CCM), Stanslaus Mabula.

Mabula alisema serikali ilishafanya mazungumzo na wananchi na kusema itachukua si zaidi ya mita 700 za wananchi waishio jirani na kiwanja hicho na kitawalipa fidia.

"Ila sasa imeonekana serikali itachukua eneo zaidi ya hilo na itazihusisha kata tano na baadhi ya kata hizo ni Shibula na Bulyahulu ambazo zaidi ya wakazi 1,400 watahusika. Je, hatua hii haitaleta athari kwa wananchi na ni lini serikali itakifanya kiwanja hicho cha ndege cha Mwanza kiwe cha kimataifa?" alihoji.

Kihenzile, akijibu maswali hayo, alisema ili kukifanya kiwanja hicho kuwa cha kimataifa, tayari serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwamo kuendelea sasa na hatua za ndani za nyaraka na uboreshaji wa sheria.

Alisema hatua nyingine ni kuondoa zaidi ya wavamizi 1,000 kwenye uwanja huo ili kuwe na usalama.

"Tunafanya kazi ya uboreshaji miundombinu. Machi 28, 2024 Waziri Prof. Makame Mbarawa alikwenda kushuhudia utiaji saini wa ujenzi wa jengo la abiria ikiwa ni hatua za kufanya uwanja huu kuwa wa kimataifa," alisema.

Kihenzile alisema kutokana na kutaka kuupa hadhi uwanja huo kuwa wa kimataifa lazima watu hao wapishe eneo hilo.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Ilemela (CCM), Dk. Angeline Mabula, alihoji ni lini mgogoro kati ya wananchi wa Kiwanja cha Ndege Mwanza na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) utatatuliwa.

Akijibu swali hilo, Kihenzile alisema serikali kwa kushirikiana na serikali ya mkoa ina nia ya dhati na imeendelea na jitihada mbalimbali katika kushughulikia mgogoro huo kuhakikisha unaisha.

Utaratibu wa kutwaa ardhi, alisema unaendelea kwa kufanya uthamini wa mali za wananchi na pindi hatua hiyo ikikamilika, taratibu zingine zitaendelea kulingana na sheria ya ardhi pamoja na sheria ya uthamini.

# Makundi ya WhatsApp kusajiliwa kisheria

**Na Romana Mallya**

MSAJILI wa Jumuiya za Kiraia katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Emmanuel Kihampa, amesema kampeni ya usajili wa jumuiya zisizo za kidini iliyoanza mkoani Dar es Salaam, inahusisha vyama au vikundi vikiwamo vinavyoendeshwa kwa njia ya mtandao wa WhatsApp.

Amesisitiza kuwa ni muhimu vyama na vikundi ambavyo watu wanakusanyika kwa lengo la kufanya sherehe au kuzungumza wakasajili.

Kwa mujibu wa Kihampa, wasiojisajili kwa mujibu wa Kifungu cha 40 cha Sheria Na.3 ya Mwaka 2019 iliyofanyia marekebisho Sheria ya Jumuiya Sura Na. 337, kuendesha chama au kikundi chenye sifa ya kusajiliwa bila kusajili ni kosa kisheria.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu kuanza kwa kampeni hiyo, Kihampa alivitaka vyama na vikundi kujitokeza katika ofisi za wilaya husika ambako ndiko usajili huo unafanyika.

"Kuendesha kikundi ambacho hakina usajili, kulingana na kosa ambalo chama au kikundi itafanya maana yake watakuwa wamevunja sheria ya nchi. Madhara yatakayotokea yatatokana na uendeshaji wa chama kwa kwenda kinyume cha sheria.

"Wasisubiri mpaka wachukuliwe hatua za kijinai, hivyo ni vyema wakaja kusajili ili waendeshe shughuli zao vizuri. Kuendesha mikusanyiko bila kufuata sheria ni kosa, ni vyema wakajiepusha na makosa haya.

"Umuhimu wa kusajili vyama na vikundi ni kuimarisha umoja na mshikamano katika taifa. Ni muhimu vyama na vikundi ambavyo watu wanakusanyika kwa lengo la kufanya sherehe au kuzungumza wakasajili vyama na vikundi vyao," alisema.

Alisema ofisi yake imewahi kusajili kikundi kinachokutanisha askari waliopigana vita kuu ya pili ya dunia ambao hukutanika na kuzungumza na kubadilishana mawazo.

Alisisitiza kuwa vikao vingi vya namna hiyo ambavyo huvisajili na kusisitiza kuwa mchakato wa usajili kuanzia mwanzo hadi mwisho ni Sh. 200,000 tu.

Kuhusu usajili ulioanza jana mkoani Dar es Salaam kwa kuanzia na wilaya ya Kigamboni, Kihampa alisema utaendeshwa kwa siku mbili katika ofisi za wilaya husika.

"Wilaya ya Temeke (Aprili 4-5), Ubungo (Aprili 6-7), Kinondoni (Aprili 8-9) na kumalizia wilaya ya Ilala.," alisema.

Usajili huo, alisema unahusisha vyama na vikundi visivyo vya kidini vya kiuchumi vikiwamo vya wafanyabiashara wadogo, wanaofanya kazi katika masoko, wakulima wafugaji na wamiliki wa mashine za kusaga nafaka.

Pia alisema vyama vya madereva, utingo, bajaji na vya kijamii ni pamoja na vya kufa na kuzikana, ujirani mwema, wanaomiliki nyumba au wanaoishi kwenye maeneo ya makazi.

"Vyama au jumuiya za kiutamaduni, vyama vya kiukoo, vya kikanda au umoja unaoanzishwa kwa lengo la kudumisha mila na desturi fulani vinatakiwa kusajiliwa," alisema.

Kihampa alitaja kundi la mwisho ni la jumuiya za kiraia zisizo za kidini zitakazosajiliwa ni vya kitaaluma vikiwamo vya wahitimu wa shule au vyuo vya elimu ya juu au stadi za ufundi.

Umuhimu wa usajili vyama au vikundi, alisema ni wanachama kupata uhalali wa kisheria kwa kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 40 cha Sheria Na.3 ya Mwaka 2019, ni sharti la lazima kusajili mikusanyiko au vyama vyote vinavyopaswa kusajiliwa kwa mujibu wa sheria hii.

Alisema umuhimu wa pili ni kutoa hakikisho kwa kulinda mali na fedha za wanachama na kuhakikisha chama kinaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kulinda maslahi na ustawi wahusika katika kikundi.

Kwa upande wa serikali, alisema umuhimu ni kupata takwimu sahihi na mtawanyiko wa vyama na vikundi vilivyoko ili kuweza kupanga mipango na mikakati mbalimbali ya kuwafikia wananchi.

Kihampa alisema kwa upande wa jamii, kuna umuhimu mkubwa wa kusajili vyama hivyo kwa kuwa, vinalenga kuongeza tija na ufanisi, kwa wizara za kisekta kuwafikia na kuwapatia mafunzo pindi inapohitajika.

"Tunatambua vyama na vikundi hivi vipo katika jamii, lakini havijasajiliwa na wengine inawezekana hawajui kabisa kama wanatakiwa kusajiliwa au kama wanatakiwa kusajiliwa waje na nyaraka zipi," alisema.

Alisema katika kampeni hii wale watakaotimiza baadhi ya nyaraka watapatiwa usajili wa haraka na moja ya nyaraka ni barua kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya husika wanakotoka.

# Washtakiwa walalamikia barua kutojibiwa

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa utetezi katika kesi inayomkabili Respicius Magesa na wenzake wanaodaiwa kujipatia Sh. milioni 159.5 kutoka akaunti binafsi ya benki ya CRDB ya Dola za Marekani na kuziingiza katika akaunti ya Shule ya Sekondari Maxmillan umedai kuwa umeandika barua mbili lakini hazijapata majibu hadi sasa.

Aidha, umedai kuwa barua hizo moja iliandikwa kwenda Ofisi ya Mashitaka ya Taifa na nyingine Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, hivyo wanataka majibu ya barua hizo.

Madai hayo yalitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Aaron Lyamuya wa mahakama hiyo na Wakili wa Serikali Frank Rimoy wakati kesi hiyo ilipofikishwa kwa ajili ya kutajwa na kuangalia kama upelelezi umekamilika au la.

Wakili Rimoy alidai kuwa bado wanaendelea na upelelezi, hivyo aliiomba mahakama iwapangie tarehe nyingine ya kutajwa.

Baada ya Rimoy kudai hivyo, Wakili Joseph Msengesi, anayewatetea washtakiwa hao, alidai kuwa kuna barua waliiandika Februari 12,2024 kwa upande wa mashtaka wakitaka kuondolewa kwa kosa la utakatishaji fedha linalowakabili lakini hadi sasa hawajapata majibu.

"Barua nyingine ililetwa na ilipokelewa mahakamani hapa. Tunaomba upande wa mashtaka ulete majibu ya barua hizo kwa sababu ukiyapitia mashtaka yote hayana uwiano na mashtaka waliyoshitakiwa nayo," alidai Msengesi.

Akijibu hoja hiyo, Wakili Rimoy alidai kuwa hawajapata barua yoyote kutoka upande wa utetezi, hivyo aliwaomba kulifuatilia barua hizo.

Hakimu Lyamuya alisema kutokana na kesi hiyo kushindwa kusikilizwa mara mbili mfululizo kutokana na shida ya mtandao, ndiyo maana wamefikishwa mahakamani, hivyo tarehe itakayopangwa kesi hiyo itasikilizwa kwa njia ya mtandao.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Aprili 9, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa. Washtakiwa wote wamerudishwa rumande kwa sababu shitaka la utakatishaji fedha halina dhamana kisheria.

Mbali na Magesa, washtakiwa wengine ni Dereva wa CRDB, Michael Owiti, wafanyakazi wa benki, Sia Meta na Ray Nittu, mfanyabiashara Aisha Bagasha, Deogratius Rulangalanga, Andrew Kamugisha na Ezekiel Salakana.

Katika kesi ya msingi , washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka ya kuongoza genge la uhalifu, kuingilia mfumo wa kompyuta, kughushi, kuwasilisha nyaraka ya uongo, kujitambulisha na kutakatisha fedha.

Ilidaiwa kuwa kati ya Julai 20 na Oktoba 29, 2023 washtakiwa wakiwa maeneo tofauti ndani ya mkoa wa Dar es Salaam, kwa nia ovu, waliongoza mtandao wa kihalifu kwa kufanya vitendo vya udanganyifu na kujipatia Sh milioni 159.5.

Ilidaiwa kuwa Nittu, akiwa Ofisa Mauzo wa CRDB Tawi la Mwenge, Julai 20, 2023 aliingilia mfumo wa kompyuta na kugushi akionyesha Kepha Mwiti amebadilisha taarifa zake za benki kwenye akaunti yake binafsi ili zifanyiwe kazi wakati akijua taarifa hizo ni za uongo.

Shtaka la sita la utakatishaji fedha, linawakabili washitakiwa wote wanaodaiwa kuwa Julai 25 na Septemba 29, 2023 wakiwa ndani ya mkoa wa Dar es Salaam walijipatia kiasi hicho cha fedha wakati wakijua ni mazalia ya kosa tangulizi la kughushi nyaraka.

CRDB BANK
*The bank that listens*

## PROVISION OF EMPLOYEE WELLNESS PROGRAM 2024-2026

**INTRODUCTION:**

CRDB Bank Plc would like to invite prospective proponents to submit proposals for the provision of Employee Wellness Program for 2024/2026.

**OBJECTIVES:**

The objective is to engage a qualified wellness Consultant who will partner with CRDB Bank in fostering a workplace culture of wellness to increase productivity and welfare of the employees.

**KEY FOCUS AREAS**

1. **Professional Telephone Counselling in Swahili and English** -
   Counselling for psychosocial problems, substance abuse and addiction, relationship problems, financial management, health, personal, or work-related problems and all mental disorders.
2. **Professional Face to Face Counselling** -
   For any psychological, relationship, medical, stress, financial problem, marital & pre-natal counselling, trauma focused counselling, teenage counselling, family therapy, individual and corporate coaching, fitness, nutrition, and lifestyle management.
3. **Managerial Consultation**
   Managerial consultancy for stress management, crisis management, assistance in managing risk cases, cultural diversity, or performance management of employees.
4. **Psychiatric Care Arrangement**
   Outpatient assessment and care through accredited Psychiatrist.
5. **Emergency Response Critical Incident Stress Debriefing (CISD)**
   Worksite Counseling and Stress Management Support such as armed robbery, death, or disaster at a worksite.
6. **Education Support and Awareness –**
   Conduct awareness program across the network to equip employees on key psychological threat / sign periodically.
7. **Home Based Care Services –**
   Support of home health services where needed.
8. **Physical wellness -**
   Support physical wellness that encourages the balance of physical activity, nutrition, good sleep, and mental well-being.
9. **Wellness Days** –
   Support in conducting annual wellness days across the network that helps to keep employees well educated in various health issues etc.
10. **Monitoring & Reporting –**
   Monthly, Quarterly & Annual
11. **Submission of Tenders -**
   All tender submissions must be online.
   Emails where tenders should be sent reads as below, any email sent sizes should be 4MB or less.
   - procurementdesk@crdbbank.co.tz
   - tenders@crdbbank.co.tz

   As part of the technical and financial evaluation of proposals, please indicate the following details in your proposal:
   i. Submit a Company Profile
   ii. Submit a detailed relevant experience with evidence attached, at least three (3) Contracts, LPO, Recommendation letters) including customers served before and type of work undertaken.
   iii. Submit at least three (3) Recommendation letters for customers served before and type of work undertaken.
   iv. Location of regional offices (HQ & Branches if Any)
   v. Annual reports / audited financial reports for the past three (3) years.
   vi. Current Annual return certificate, for Tanzania companies, this is obtained from BRELA.
   vii. Submit legal and business certificates.
   viii. Submit valid Regulatory, Government Board or Agency certificate required for such goods/services.
   ix. Submit Valid Business license.
   x. Employees CVs & certificates
   xi. The following forms are available in our website for filling and submitting as part of the requirements, vendor application, Non-disclosure agreement and Bank indemnity form.
12. **Deadline of submission to be indicated as**
   - Tender deadline for submission 05th April 2024
   - Tender Closing time 12:00 hrs
   - Tender opening time 16:00 hrs (a link will be sent through to the email that submitted the tender)

**The Managing Director**
CRDB Headquarters,
Plot No.25 & 26 Ally Hassan Mwinyi Road &
Plot No.21 Barrack Obama Road
P.O. Box 268, 11101 Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 (0) 22 211 7441 – 7
Fax: +255 (0) 22 211 6714
Email: info@crdbbank.co.tz
Website: http://www.crdbbank.co.tz

# TRA yakusanya Trilioni 6.63/- katika robo ya tatu 2023/24

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imekusanya Sh. trilioni 6.63 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2023/24.

Kiasi hicho ni sawa na ufanisi wa asilimia 95.17 ya lengo la kukusanya Sh.trilioni 6.97.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma jana na mamlaka hiyo, makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia 11.68 kulinganishwa na makusanyo ya Sh. trilioni 5.94 ya kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2022/23.

Taarifa hiyo ya TRA ilibainisha kuwa kwa mwezi Machi 2024, mamlaka hiyo ilikusanya Sh. trilioni 2.49 sawa na ufanisi wa asilimia 97.5 ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 2.56. Makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia 6.91 kulinganishwa na Sh. trilioni 2.32 kilichokusanywa mwezi kama huo mwaka 2023.

TRA ilifafanua katika taarifa yake hiyo kuwa mafanikio yaliyofikiwa katika kipindi cha robo tatu ya mwaka wa fedha 2023/24 yamechagizwa na kuongezeka kwa uhiari wa ulipaji kodi kufuatilia maboresho yanayoendelea kufanywa ikiwamo kusogeza huduma jirani na walipaji kodi kwa kuanzisha divisheni za walipakodi wadogo na walipakodi wa kati pamoja na kuendelea kusuluhisha pingamizi za kodi nje ya mahakama.

"Mwitikio mzuri wa walipakodi kuwasilisha kwa wakati ritani za kodi kwa mwaka 2024 kupitia mifumo ya Tehama ya uwasilishaji wa ritani, kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji na ukuaji wa shughuli za kiuchumi nchini zinazochangia mapato kama vile sekta za madini, taasisi za kifedha zikiwamo benki na sekta ya utalii pia kumechagiza mafanikio hayo," TRA ilibainisha katika taarifa yake hiyo.

Pia ilitaja kuongezeka ufanisi katika huduma za forodha hususan katika kusimamia kodi zinazohusiana na uingizaji mizigo kutoka nje ya nchi kuchagiza mafanikio hayo.

Katika kuhakikisha lengo la makusanyo ya kodi kwa mwaka 2023/24 linafanikiwa, TRA ilisisitiza wananchi kuendelea kutoa taarifa kuhusu vitendo vinavyoashiria ukwepaji kodi, ikiwamo biashara za magendo na uuzwaji wa bidhaa ambazo hazijapandikwa stempu za kielektroniki.

"Ikumbukwe kuwa kukithiri kwa vitendo hivi hakuathiri tu makusanyo ya serikali, bali pia kunaathiri afya na usalama wa wananchi kwa bidhaa hizo kuuzwa sokoni wakati hazina viwango vya ubora kwa matumizi ya binadamu," TRA ilitahadharisha katika taarifa yake hiyo.



Baadhi ya wajasiriamali wanawake wa Kata ya Kipunguni, jijini Dar es Salaam, wakiwa kwenye kikao cha kuweka mikakati ya kuwawezesha kuwania uongozi, katika uchaguzi wa serikali za mitaa, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mabinti 63 wa mazingira magumu wakopeshwa mtaji wa milioni 100/-

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WASICHANA 63 kutoka familia zenye mazingira magumu ndani ya kata tatu za Manispaa ya Morogoro wamepata elimu ya ujasiriamali na mitaji yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya kuanzisha viwanda vidogo kwa kukuza uchumi wao na kutimiza dhana ya Serikali ya Tanzania ya Viwanda.

Meneja wa Shirika la Kuhudumia viwanda vidogo (SIDO) mkoani Morogoro, Joan Nangawe, alisema hayo jana wakati wa hafla ya kuwaaga wasichana hao wenye umri kuanzia miaka 12 na kuendelea walipopatiwa vyeti na vifaa mbalimbali vya saluni, vyerahani na mapishi baada ya kuhitimu mafunzo ya miezi mitatu.

Nangawe alisema SIDO imetoa elimu kwa wasichana hao kutoka kata za Mwembesongo, Tungi na Kingolwira baada ya ushirikiano baina yao na shirika linalojihusisha na masuala ya kifedha la Brac Maendeleo tawi la Msamvu mjini hapa.

Alisema SIDO itaaendelea kuwalea, kuwafuatilia na kuwashauri wasichana hao ili wafanye kazi kwa kuzalisha na kuajiri vijana wengine lengo likiwa ni kuchangia uchumi wa taifa na wao mmoja mmoja. "Vijana hawa wanapata mafunzo ya aina mbalimbali kwa muda wa miezi mitatu ikiwamo ushonaji, mapambo na urembo, mapishi na usindikaji wa chakula," alisema.

Alisema SIDO inatambua kuwa serikali imeweka juhudi kubwa kuhakikisha vijana wanapata elimu huku wakiwa na miundombinu wezeshi ya kujenga uchumi endelevu na SIDO imekuwa ni sehemu ya mchango huo ambayo imehakikisha wamepata teknolojia sahihi zitakazowawezesha kufanya kazi zenye tija na kufahamu wapi fursa ipi inapatikana.

Akifunga mafunzo hayo Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mhandisi Pascal Kihanga, aliwashauri wasichana hao kujiunga katika vikundi na kuanzisha viwanda vya pamoja jambo litakalowasaidia kupata fedha za mikopo kutoka Halmashauri na kwingine na kuzidi kukua kiuchumi.

Mhandisi Kihanga alisema halmashauri hutenga asilimia 10 kwa kila mapato ya mwaka wanayopata na mwaka wa fedha 2025 watakusanya zaidi ya Sh. bilioni 15 na asilimia 10 itakwenda katika mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu ambapo wanawake hao nao watafaidika.

Aliwasihi wanawake hao watakapopata mikopo hiyo ambayo haina riba kutoka manispaa kurejesha kwa wakati kama walivyofanya wanawake waliokopeshwa awali ambao walirejesha kwa wakati, lakini tatizo lilikuwa kwa vijana ambao walikuwa hawarejeshi.

Meneja wa Mradi wa kuwezesha wanawake vijana kiuchumi kutoka Shirika la Brac Maendeleo tawi la Msamvu, Grace Mtunguja, alisema kati ya wasichana 63 waliopatiwa mafunzo hayo 34 walichukua fani ya ushonaji, wanafunzi 25 walichukua fani ya saluni na mapambo, wengine 19 walijikita kwenye upishi.

Alisema mradi huo ni endelevu kwa muda wa miaka mitano kuanzia mwaka 2023/27 ambapo wataendelea katika kata zingine ikiwemo kata za kichangani na Mji mpya wakianzia kuwapata wasichana hao kutoka familia zisizojiweza kichumi kupitia kwenye ofisi za kata husika lengo likiwa ni kumfanya mama awe na ajira inayotambulika.

## KUPOTEA KWA HAKI HATI YA KIWANJA.

**SARAH LAZARO KEIYA** anatangaza kupotea kwa Haki Hati ya kiwanja Na. **705 Kitalu -H, Njiro-Arusha.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA PHQ/ARU/ARU/5180/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**TATU SAIDI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P2517-0547** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ALFA SECONDARY SCHOOL CENTRE** mwaka 2017.kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MOR/MOR/RB/543686/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMED OMARY MTIGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MERCEDEZ BENZ ACTROS** yenye jina la umiliki **ROADGRIP 2020 LIMITED** lenye usajili namba **T 123 DVF,** CHASSIS NAMBA : **WDB9542332K7675D8.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/47644/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DENIS FESTO NJAU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0920/0040** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **PAKULA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2011. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/4997/2024**

**IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE N. 2048 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late of the late MELKION ADAM NDOMBA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY BUNGA IDDY RAMADHANI AND JOHN ADAM RAMADHANI**

**GENERAL CITATION (Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 16 Day of 4, 2024

Dated at Dodoma this 27 Day of 3, 2024.

PRINCIPLE/RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA CHETI



**OMARY S ALLY** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1818-0161-2012** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia SHULE YA SEKONDARI BARAA mwaka 2012. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIG/41471/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAMWEL EDWARD MUGOYE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 347 DVN.** Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/IRI/IRI/3982/2024**

TANGAZO


Nipashe
MWANGA WA JAMII
Kesho Ndio Siku Yetu!!
Jambo letu Sote
iPP
CARES FOR YOU
The Guardian
www.ippmedia.com

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hadhari ichukuliwe dhidi ya mvua inayoendelea sasa

**MVUA** ya masika imeendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini. Kama ilivyotabiriwa na mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania (TMA) katikati ya mwezi uliopita, mvua hiyo imenyesha kwa kiwango kikubwa kwenye mikoa ya Pwani ya Bahari ya Hindi ikiwamo Dar es Salaam, Morogoro, Lindi na Mtwara pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba.

Katika baadhi ya mikoa kama Lindi na Morogoro, yameripotiwa maafa yakiwamo kukatika kwa mawasiliano ya usafiri baada ya miundombinu kuharibiwa huku kaya kadhaa zikikosa makazi na mahitaji muhimu baada ya nyumba kuharibiwa na zingine kubomoka kabisa.

Mkoani Morogoro, kwa mfano, mvua iliyoanza kunyesha mwishoni mwa wiki iliyopita juzi ilisababisha nchi kuwa gizani kwa takriban saa 12 baada ya mitambo ya kuzalisha umeme ya Kidatu, kuingia maji yaliyozidi kipimo. Hatua hiyo ilisababisha mfumo wa uzalishaji umeme kuharibika na kuathiri gridi ya taifa.

Pia katika mkoa huo, mvua inayoendelea kunyesha, imesababisha mawasiliano kukatika katika Halmashauri ya Mlimba wilayani Kilombero baada ya maji ya mvua kuharibu Barabara na kuvunja daraja. Maafa mengine yaliyoripotiwa ni njia ya reli ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zanzibar (TAZARA) ambayo imeharibika, hivyo kuwapo kwa ugumu wa treni kupita kutoka au kwenda Zambia.

Mkoani Mtwara pia kumeripotiwa kuwapo kwa maafa ya mvua katika wilaya ya Nachingwea. Mvua hiyo imeelezwa kubomoa nyumba na kuharibu mali na makazi ya watu, huku waathirika wakiomba serikali kuwapatia msaada. Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Mohamed Moyo, takriban kaya 1,660 zimeathirika na mvua hiyo huku nyumba 699 zikibomoka kabisa.

Maafa yaliyoripotiwa yametokea chini ya wiki tatu baada ya mvua kubwa kunyesha katika mikoa ya Lindi na Mtwara iliyosababisha Daraja la Nanganga kusombwa na maji hatimaye kuwafanya wananchi waliokuwa wakisafiri kutoka au kuingia katika mikoa hiyo kukosa usafiri. Hatua hiyo ilisababisha Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, kuweka kambi na kikosi maalum cha ujenzi ili kurejesha hali ya miundombinu na kuwezesha usafiri kurejea.

Kama ilivyotangaza TMA, mvua hiyo inatarajiwa kuendelea kunyesha hadi katikati ya Mei, hivyo kuna uwezekano mkubwa wa kutokea maafa kama ambavyo imetokea katika maeneo mengine yaliyotajwa.

Kutokana na umuhimu huo, hatua mbalimbali zinapaswa kuchukuliwa ili kuepusha madhara makubwa katika jamii ikiwamo wananchi kukosa makazi, kukosekana kwa usafiri na usafirishaji kutoka sehemu moja kwenda nyingine na hata kuwapo kwa vifo vya watu na upotevu wa mali.


Hulka ya wengi ambayo imezoeleka ni kwamba kumekuwa na mtindo wa watu kudharau tahadhari zinazotolewa kuhusu matishio ya kutokea kwa majanga. Matokeo yake, watu wamekuwa wakipoteza maisha, mali yakiwamo mazao kusombwa na mafuriko na nyumba kuzingirwa na maji na kubomoka.

Mbali na madhara hayo, pia kumekuwa na magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu, homa za matumbo , kuhara na kuhara damu katika baadhi ya maeneo, Dar es Salaam ikiwamo, kutokana na mifumo ya majitaka kutokuwa thabiti, hivyo kuruhusu maji machafu kusambaa na watu kuyatumia bila kuchukua tahadhari.

Kama wahenga wasemavyo mdharau mwiba mguu huota tende, ndivyo inavyotokea kwa watu ambao hawachukui hatua pindi hadhari za majanga zinapotolewa. Ni vyema sasa jamii ikabadilika kwa kuchukua hadhari dhidi ya majanga.

Ili kudhibiti madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na mvua hiyo, ni muhimu hatua zikachukuliwa kuanzia mtu mmoja, kaya hadi mamlaka zilizopewa dhamana ya kusimamia miundombinu na mazingira. Bila maafa ya mvua Tanzania inawezekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Umaskini na siasa vinaweza kukwamisha chakula shuleni

**TANGU** mwaka 2016, serikali inaendelea na utaratibu wa utoaji elimu bure ikiwa imeanzia shule ya msingi hadi kidato cha nne lakini baadaye ikaunganisha hadi kidato cha sita.

Hatua hiyo imesaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari ambao ni matokeo ya elimu bure, kutokana na kwamba hakuna ada ambayo huenda ingekuwa ni kikwazo.

Pamoja na utaratibu huo wa elimu bure, linakuja suala la chakula shuleni ambalo wazazi na walezi wanapaswa kila mmoja kuchangia ili watoto wapate angalau mlo mmoja wawapo shuleni.

Hata hivyo, kuna kusuasua katika uchangiaji wa chakula shuleni, kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo baadhi ya wazazi na walezi kukosa fedha za kuchangia na kudai serikali ishatangaza elimu bure.

Wapo wengine ambao wanarubuniwa na wanasiasa kwamba suala la kuchangia chakula shuleni ni jukumu la serikali, hali ambayo inasababisha uchangiaji kusuasua kwa huduma hiyo shuleni.

Ni kweli inawezekana wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao hawana uwezo wa kuchangia fedha kwa ajili ya chakula cha watoto wao shuleni, lakini ninadhani wanaweza kuchangia chakula badala ya fedha.

Kama mzazi au mlezi ana maharage au mahindi kutoka shambani mwake, anaweza kuchangia badala ya kudai hana fedha wakati ana chakula kitendo ambacho binafsi ninaona si sahihi.

Hivyo, wale ambao hawana fedha lakini wana chakula, ni vyema wakakipeleka shuleni, wasio na kipato, nao ijulikane kwamba hawana kuliko kuendelea na visingizio huku watoto wao wakiumia.

Ninaamini kuwa chakula shuleni kinaongeza usikivu darasani, hivyo, jamii ingeacha visingizio na badala yake, kila mmoja afanye sehemu yake kwa chochote alicho nacho kusaidia mtoto wake.

**Pamoja na hayo, ninadhani si sahihi wanasiasa kuingilia uchangiaji chakula shuleni na kushawishi wazazi na walezi wasichangie, huku wakiwa na ajenda yao ya kisiasa.**

Hivyo, ukosefu wa kipato kwa baadhi ya wazazi na walezi usiwe kikwazo kwao kuchangia chakula, ni vyema wakatambua kuwa si lazima kuchangia fedha tu bali hata chakula chenyewe.

Mtu anaweza akawa hana fedha, lakini akawa na mavuno kutoka shambani mwake, akatoa kiasi na kupeleka shuleni kwa ajili ya huduma ya chakula ya mtoto wake au watoto wake.

Ninaamini kwamba kila mmoja anaweza kushiriki kwa namna moja au nyingine kuwezesha chakula shuleni badala ya kujiweka pembeni na kudhani ni jukumu la serikali au kuegemea kwenye umaskini.

Pamoja na hayo, ninadhani si sahihi wanasiasa kuingilia uchangiaji chakula shuleni na kushawishi wazazi na walezi wasichangie, huku wakiwa na ajenda yao ya kisiasa.

Imekuwa ikidaiwa kuwa baadhi ya wanasiasa huwaambia wananchi kuwa wasichangie chakula shuleni, kwa maelezo kwamba hilo ni jukumu la serikali, kitendo ambacho kinachangia kukwamisha huduma hiyo.

Kutokana na mkanganyiko huo, ninadhani ipo haja ya kutolewa elimu kwa umma kujua umuhimu wa kuchangia chakula shuleni, kwani wataalam wa afya huwa wanasema, chakula shuleni kinaongeza ufaulu.

Wanasema, kuna uhusiano kati ya afya ya mwanafunzi na maendeleo yake kitaaluma, hivyo, kuna haja ya kutolewa elimu ili jamii ielewe umuhimu huo na kuacha upotoshaji.

Jamii ikielimishwa, inawezekana wakazi wa vijijini, wakati wa mavuno, wazazi na walezi wanaweza kuwasiliana na walimu ili kujua bajeti ya mtoto awapo shuleni na kuweka utaratibu wa chakula kutunzwa shuleni.

Ikumbukwe kuwa serikali imeshaelekeza kuwa ni lazima mtoto apate chakula, hivyo ile bajeti yake ambayo angekula akiwa nyumbani ipelekwe shuleni, ili aweze kupata chakula awapo huko.

HABARI KITAIFA

# Mikakati kukabiliana upungufu walimu yatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetaja mikakati ya kukabiliana na upungufu wa walimu wa shule za msingi na sekondari nchini na kuwataka Wakurugenzi wa Halmashauri kuzingatia mwongozo wa kutoa ajira za mkataba ili kunusuru hali hiyo.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk.Festo Dugange, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Vwawa (CCM), Japhet Hasunga.

Katika swali lake, alihoji serikali inachukua hatua zipi za muda mfupi, kati na mrefu kutatua upungufu huo.

Dk. Dugange alijibu kuwa serikali imeajiri walimu kwa wingi wa sayansi na biashara na itaendelea kuajiri kadri kibali cha ajira kinavyotoka ili kupunguza upungufu.

"Pia, serikali ilitoa mwongozo wa jinsi ya kuajiri kwa mkataba na niombe wakurugenzi waajiri kwa kufuata mwongozo huo," alisema.

Katika swali la msingi, alihoji serikali ina mkakati gani kupeleka walimu wa kutosha katika shule za msingi na sekondari mpya 10 zilizojengwa Vwawa.

Dk. Dugange akijibu swali hilo, alisema serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi imeshapeleka walimu 33 kwa shule mpya za msingi na walimu 32 kwa shule mpya za sekondari ili wanafunzi wapate masomo.

Hata hivyo, alisema serikali kila mwaka inaendelea kupunguza mahitaji ya walimu katika sekta ya elimu na hivi karibuni itatangaza ajira za walimu baada ya taratibu za kibali kutoka Ofisi ya Rais – Utumishi kukamilika na kadri ya upatikanaji wa fedha.

**Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk.Festo Dugange, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Vwawa (CCM), Japhet Hasunga.**



Watoto wenye usonji wakiandamana kuelekea Msimbazi Mseto, jijini Dar as Salaam jana, wakati wa siku ya usonji Duniani, iliyoandaliwa na Lukiza Autism Foundation. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maduka ya kubadili fedha za kigeni yaliyofungwa kurudishiwa fedha zao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Fedha imeeleza kuwa maduka saba ya kubadilishia fedha za kigeni kati ya 68 yaliyokuwa yamefungwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) tangu mwaka 2018 na 2019, yako mbioni kufunguliwa na wamiliki wake watarudishiwa mali na fedha zilizochukuliwa na serikali.

Maduka hayo ni yale yaliyokuwa yamesalia kufunguliwa baada ya kufungwa katika ukaguzi maalum uliofanywa na BoT kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za serikali, wakibaini makosa mbalimbali.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Chumbuni (CCM), Ussi Salum Pondeza.

Mbunge huyo alisema kuna maduka ambayo yamefungwa na ikajulikana hayana makosa ya utakatishaji fedha na kuhoji kama serikali iko tayari kuwarudishia fedha na mali zao zilizochukuliwa na serikali kwa wale ambao walifungiwa na hawana tuhuma za utakatishaji fedha.

"Ni lini wale wote ambao walikuwa wameonekana hawana hatia maduka yao yatafunguliwa?" mbunge huyo alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Chande alisema maduka yaliyofungwa katika ukaguzi huo yalikuwa 68 na yaliyobaki ambayo hayajafunguliwa hadi sasa ni saba.

"Maduka haya saba yatafunguliwa muda wowote, nikuhakikishie kuwa serikali chini ya uongozi wa Rais Samia haiko tayari kuona kuna rasilimali fedha ya mtu imebaki serikalini kumnyima mtu haki yake," alisema.

Naibu Waziri Chande alisema wale wote ambao wameonekana maduka yao hayana makosa yoyote, watarudishiwa fedha zao na rasilimali zingine zote.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba pia aliongeza majibu, akisema "Serikali ya awamu ya sita haiko radhi kuona fedha za raia mwema zinashikiliwa na serikali na kulikuwa na kodi ambayo ilikuwa imezidishwa, tayari imesharejeshwa kwa wale waliokuwa wanahusika.

"Kama alivyosema Naibu Waziri tutaendelea kwa wale ambao watakuwa na baadhi ya vitu vilikuwa kwenye mikono ya serikali."

Katika swali la msingi, Mbunge Pondeza alihoji sababu za maduka ya kubadilisha fedha kuondolewa katika biashara na wananchi wengi kupoteza ajira zao.

Naibu Waziri Chande, akijibu swali hilo, alisema kuwa mwaka 2016, BoT ilifanya ukaguzi wa maduka hayo na kugundua miamala mbalimbali kwa baadhi ya maduka kufanyika kinyume cha matakwa ya sheria na kanuni za usimamizi wa maduka ya fedha za kigeni.

Alitaja makosa yaliyobainika kwenye ukaguzi huo kuwa ni kutofanya utambuzi wa wateja kabla ya kutoa huduma kinyume cha kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji Fedha Haramu, Sura 423 na kanuni ya 17 ya Kanuni za Udhibiti wa Utakatishaji Fedha Haramu; kugawa miamala ya wateja kwa lengo la kukwepa kutunza kumbukumbu muhimu zinazoonesha uhalali wa miamala kinyume cha Kanuni ya 23(4) ya Kanuni za Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni ya mwaka 2015.

Pia alitaja dosari ya kutokutoa stakabadhi za miamala kinyume cha Kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni ya mwaka 2015; kutokuwasilisha taarifa sahihi za miamala Benki Kuu na hivyo kuathiri upatikanaji takwimu muhimu kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na baadhi ya maduka yalikuwa yanajihusisha na uhamishaji fedha nje ya nchi bila kuwa na leseni wala kibali cha Benki Kuu.

Alisema kuwa baada ya operesheni hiyo, BoT ilibatilisha leseni za maduka ya kubadilisha fedha za kigeni yaliyokutwa na makosa.

"Uamuzi huo ulifanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 36(1)(b) na 2(d) ya Kanuni za Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni ya Mwaka 2015 iliyorejewa mwaka 2019," alisema.

KABWELA FADHILI MOHAMED



# Bunge lajiondoa KADCO kusaini notisi ya KIA

**Na Vitus Audax,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ametoa ufafanuzi kuhusu uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) kuwa upo chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Nchini (TAA) kama ilivyoazimiwa na Bunge, Novemba 2023.

Kadhalika, amesema suala la Kampuni ya Uendelezaji na Uendeshaji Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KADCO) iliyokuwa inasimamia uwanja huo, kutia saini barua ya notisi kwa waliovamia eneo hilo badala ya TAA lipo ndani ya kiutendaji wa serikali na Bunge limeshamaliza kazi yake.

Dk. Tulia alitoa kauli hiyo jana bungeni kutokana na kusambaa kwa barua ya notisi hiyo iliyotolewa Machi 10, 2024 na kampuni hiyo ya KADCO wakati Bunge lilishaazimia KIA ipo chini ya usimamizi wa TAA na limeshuhudia makabidhiano.

Alisema kutokana na makabidhiano hayo wananchi walitaraji barua hiyo iandikwe na TAA na sio KADCO kama ilivyosambaa ikiwa na saini na mihuri ya kampuni hiyo.

Alisisitiza kuwa jukumu la Bunge juu ya makabidhiano ya kiwanja hicho kwa Mamlaka husika liliisha mwezi Novemba, 2022 na 2023 baada ya Bunge hilo kuazimia kiwanja hicho kutoka kwenye uendeshaji wa Kampuni ya KADCO.

Alisema baada ya maadhimio hayo ambayo yalikwama kutekelezwa mwaka 2022 kutokana mkataba mmoja wa upangaji uliokuwa bado ukikwamisha, mwaka 2023 Bunge hilo liliridhia mkataba huo usiwe kikwazo kutokana na kampuni hiyo kumilikiwa na serikali kwa asilimia 100.

Pia, alisema lilitolewa tamko la serikali kutoka kwa Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa Novemba 9, mwaka jana kuwa kikabidhiwe kwa TAA kama viwanja vingine vinavyoendeshwa.

"Serikali ililifanyia kazi suala hilo na wajumbe wa kamati yetu ya miundombinu wakiongozwa na mwenyekiti walienda kushuhudia makabidhiano kati ya TAA na KADCO yaliyofanyika Novemba 10, 2023 baada ya hapo kwa utaratibu wa kawaida Bunge linakuwa limemaliza kazi yake na mambo menginne ya kiutendaji yanakuwa ya serikali," alisema Dk.Tulia.

Kuhusu kutia saini kwa barua hiyo na KADCO, Dk.Tulia alisema Bunge haliwezi kuingilia na kujua kwanini na nani ametia saini barua kwa kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mgawanyo wa madaraka kwa mujibu wa Katiba. "Wananchi kusoma na kubaini kuwa ujumbe huo umetolewa na KADCO wameshtuka wakati Bunge lilisema hapo ni TAA na pia tayari serikali imekabidhi TAA, walitaraji barua iandikwe na TAA."

"Hivyo suala la utendaji ndani ya serikali kwa maana ya makabidhiano ya ndani yanaisha lini ni suala ambalo kama Bunge hatuwezi kuingia huko labda itokee changamoto kubwa," alisisitiza Dk. Tulia.

Alisema kuhusu mkanganyiko na mjadala wa kuwa Bunge limedharauliwa kwa KADCO kuandika barua ni mchanganyiko ndani ya serikali na wala wao hawaingii kwenye utendaji wala hakuna namna serikali itadharau na kwenda kinyume na maamuzi ya Bunge.

"Hata hivyo katika wiki chache zilizopita tumeona Mhe. Rais amechukua hatua kwa kumtoa yule aliyekuwa Mkurugenzi wa KADCO na kumpeleka AICC na hatujaona akiteuliwa Mkurugezi mwingine wa KADCO kuashiria kwamba bado ni mchakato unaoendelea kuhakikisha TAA inashika madaraka hapo KIA," alisisitiza Spika Dk. Tulia na kuwatoa wasiwasi wananchi.



Mwakilishi wa Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation (AMF), Mabrouk Aboud (wa nne kulia), akikabidhi msaada wa futari kwa kijana yatima, Tarik Hassan katika kituo cha Malaika Kids cha Mkuranga, mkoani Pwani jana. Taasisi hiyo, ilikabidhi msaada wa futari katika vituo vitatu vya kulelea watoto yatima ikiwemo mchele kilo 200, maharage kilo 90, unga wa ngano kilo 75, sukari kilo 30, mafuta ya kula lita 30 na tende boksi 20, ikiwa ni utekelezaji wa ibada ya kusaidia wasiojiweza wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadan. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Samia aridhia na kutia saini miswada sheria za uchaguzi

**Na Vitus Audax,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameridhia na kutia saini miswada minne iliyopitishwa na Bunge katika mkutano uliopita.

Hiyo ni Miswada ya: Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani; Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa; na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5, yote ya mwaka 2023.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alibainisha hayo bungeni jijini hapa jana alipotoa taarifa kwa wabunge, akisema miswada hiyo iliyopitishwa na tayari imepata kibali kutoka kwa Rais Samia na kuzifanya zote kuwa sheria za nchi, hivyo zitaanza kutumika rasmi.

"Sasa hizi zimekuwa sheria za nchi na zitaanza kuitwa kwa majina yafuatayo; Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024.

"Nyingine ni Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa Na. 3 ya Mwaka 2024, Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 ya Mwaka 2024. Kwahiyo, waheshimiwa wabunge, hizi tayari zimekuwa sheria kamili. Mheshimiwa Rais ameishafanya kwa sehemu yake," alisema Spika Dk. Tulia.

Wakati miswada hiyo inawasilishwa bungeni Novemba 10, 2023, ilizua mawazo mseto kutoka kwa wadau mbalimbali kikiwamo chama kikuu cha upinzani, CHADEMA, kilichoibuka na hoja ya kutaka iondolewe bungeni kwa kuwa haijajibu matatizo ya msingi.

Kwa mujibu wa chama hicho, miswada hiyo ilikuwa na matatizo ya msingi ya muundo wa tume pamoja na sheria za uchaguzi, hivyo kupendekeza mambo mbalimbali kufanyika ikiwamo kuondolewa kwa miswada hiyo ili iandikwe upya kwa mujibu wa marekebisho ya mpito ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 yatakayofanyika kama kilivyopendekeza.

Spika Tulia pia akifungua mkutano wa Bunge la Bajeti, akiwakumbusha wabunge kumkumbuka na kumwombea Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Ali Hassan Mwinyi na kuahidi kumkumbuka kwa utendaji wake wa kazi pamoja na uwajibikaji katika nafasi mbalimbali alizozitumikia.

Kifo cha Mzee Mwinyi, maarufu Mzee Rukhsa, kilitangazwa na Rais Samia Februari 29, mwaka huu. Mwili wake ulizikwa Machi 2, mwaka huu huko Mangapwani, Unguja baada ya kuagwa na wananchi Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na baadaye Uwanja wa Amani, Zanzibar.

## RC akabidhi msaada kwa kituo cha kulea yatima

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abass ametoa msaada wa vitu mbalimbali vyenye thamani ya zaidi ya Sh.800,000 na kutoa fedha taslimu Sh. 690,000 kwa kituo cha watoto yatima cha Chipole, wilayani Songea.

Kituo hicho chenye watoto yatima 74, kinamilikiwa na watawa wa Shirika la Mtakatifu Agnes Jimbo Kuu Katoliki la Songea.

Baada ya kukabidhi msaada huo, Kanali Abbas alivitaja vitu walivyopewa watoto hao ni mchele kilo 100, maharage kilo 50, mafuta ya kupikia lita 20, sukari kilo 50, unga wa mahindi kilo 50 na sabuni ya unga mifuko miwili.

"Mimi binafsi nimekuwa na utamaduni katika maisha yangu, nikipata fursa huwa ninatembelea vituo vya kulelea watoto yatima kwa lengo la kuwashika mkono na kuwafariji, huwa ninafarijika ninapofanya jambo hili," alisema.

Alipongeza watawa hao kwa upendo mkubwa walionao kwa kuchukua jukumu la kuhudumia watoto yatima, akisema jukumu hilo ni la Mungu.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Rehema Madenge alipongeza watawa hao kwa kulea watoto yatima 74 ambao aliwataja wako katika mikono salama kutokana na kituo hicho kuwa kimbilio la watoto wengi.

Alisema kituo hicho kinaisaidia serikali kulea watoto yatima na hakuna malipo yanayostahili kwa kazi hiyo zaidi ya kuwaombea thawabu kwa Mungu.

Ofisa Ustawi Mkoa wa Ruvuma, Victor Nyenza, akitoa taarifa ya vituo vya kulelea yatima, alisema katika mkoa mzima wana watoto yatima 279. Kati yao, watoto 74 wanalelewa katika Kituo cha Chipole.

Jumuiya ya watawa wa Chipole ilishukuru Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwa msaada wa vitu vitatu na fedha na kuwafariji na kuwatia moyo wa kuendelea kuwa na huruma na upendo wa kuhudumia watoto yatima.



## KCMC kutoa huduma za kibingwa magonjwa ya moyo

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC, inakusudia kuanzisha kitengo cha kuhudumia magonjwa ya moyo ili kutoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi kwa wagonjwa wanaougua magonjwa hayo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya KCMC, Prof. Gilleard Masenga, Juni mwaka huu wataanza ujenzi wa kitengo hicho kitakachokuwa na uwezo wa kuchukua vitanda 100 pamoja na chumba cha upasuaji na vyumba maalum.

"Serikali iko sambamba na sisi katika kuhakikisha kuwa kitengo hicho cha magonjwa ya moyo kinaenda kukamilika hivi karibuni.

"Katika nchi zinazoendelea Tanzania ni mojawapo ya nchi zinazotishiwa na magonjwa ya moyo na magonjwa yasiyoambukiza yamekuwa yakiongezeka kwa kasi.

"Hapa Hospitalini kwetu KCMC katika yale magojwa 10, ambayo watu wanalazwa mara kwa mara, magonjwa yasiyoambukiza ni manane. Nikimaanisha magonjwa ya moyo kisukari, shinikizo la damu, saratani na ajali."

Asilimia 26 ya wagonjwa wanaoenda kutibiwa katika hospitali hiyo ni wagonjwa wa moyo, ambapo vifo ni zaidi ya asilimia 20 vinavyotokana magognjwa ya moyo.

Mkurugenzi Mtendaji Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Prof, Muhamed Janabi, alisema kwa sasa tatizo la moyo ni kubwa kwa kuwa watu zaidi ya milioni 18 wana kufa kwa mwaka kwa sababu ya matatizo ya moyo

"Kwa hiyo Tanzania na sisi tupo kwenye mkondo huo na hata ukitizama takwimu zetu za nyuma asilimia kubwa ya wagonjwa wa moyo walikuwa wanapelekwa kutibiwa nje" alisema.

Alisema kuwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Hospitali ya Kibingwa ya Benjamin Mkapa na KCMC, itakapoanza kutoa huduma, itakuwa imepunguza asilimia 95 ya wagonjwa kwenda nje ya nchi kutibiwa.

**"Serikali iko sambamba na sisi katika kuhakikisha kuwa kitengo hicho cha magonjwa ya moyo kinaenda kukamilika hivi karibuni.**

# Ole Sendeka afichua sababu za kushambuliwa kwa risasi

**Na Godfrey Mushi,**
SIMANJIRO

MBUNGE wa Simanjiro (CCM), mkoani Manyara, Christopher Ole Sendeka, amefichua kile kilichojificha nyuma ya pazia kuhusu kushambuliwa na risasi akisema siku moja kabla ya tukio hilo alifanya mazungumzo na viongozi wa juu, kuhusu hatma ya ardhi ya wafugaji inayotakiwa kubadilishwa kuwa maeneo ya hifadhi.

Ole Sendeka akiwa safarini alishambuliwa kwa risasi Machi 29 mwaka huu majira ya saa 12:45 jioni katika Kijiji cha Ngabolo, Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara.

Akizungumza juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Wilaya ya Simanjiro, Ole Sendeka, alisema Alhamisi ya Machi 28 mwaka huu alikaa na viongozi kujadili suala la kupandishwa hadhi kwa mapori ya wafugaji.

"Niwape na siri nyingine. Ijumaa ndiyo nimeshambuliwa (Machi 29), Alhamisi (Machi 28), nilikaa na viongozi kujadili kupandishwa hadhi kwa mapori haya ya wafugaji. Tena viongozi wa ngazi za juu kabisa. Na tukaelewana, kila mmoja anasema hatutakubali ardhi yetu ibadilishwe kuwa ardhi ya wanyama. wamesema wenyewe.

"Lakini hii hainifanyi nisiende bungeni kusema. Ngojeni niwaambie, hotuba yangu ya kwanza bungeni haitakuwa kueleza kupigwa kwangu risasi.

...Itakuwa ni kueleza kwamba ardhi ya wafugaji wa Simanjiro, ardhi ya wafugaji wa Monduli, ardhi ya wafugaji wa Ngorongoro, ardhi ya wafugaji wa Longido, ardhi ya wafugaji wa Kiteto, ardhi ya wafugaji wa Same na Mwanga; wamependekeza nazo ziwe hifadhi katika ardhi wanazoishi wamasai."

Katika mkutano huo, Ole Sendeka, alisema atakwenda kueleza kwamba serikali ikichukua hata kilomita moja katika eneo hilo, kwa ajili ya kisingizio cha uhifadhi ni kuweka rehani maisha ya wafugaji walioko hapo, kwa sababu wafugaji watakuwa hawana maisha tena.

"Walitaka kuniondoa uhai ili niache watoto wangu wadogo. Nina uhakika serikali haina mkono katika jaribio la kutaka kuondoa maisha yangu. Wangehusika ningemtaja mmoja hadi mwingine kwa jina. Naomba tuelewane, serikali ya CCM (Chama Cha Mapinduzi) ingehusika, ningemtaja kwa jina hadharani.

Zaidi aliongeza: "Kazi iliyonayo serikali kwa sasa ni kuchunguza na kuwapata waliohusika. Wanaweza kuwa wana CCM wamefanya hilo, wanaweza kuwa watu wengine wa aina yeyote, lakini akiwa ni anayefanya kazi serikalini, akiwa ni wa upinzani, atapatikana."

Katika taarifa kwa umma iliyotolewa Machi 30 mwaka huu na Msemaji wa Jeshi la Polisi Nchini, Naibu Kamishna, David Misime, ilieleza kuwa Christopher Ole Sendeka na dereva wake (ambaye hakutajwa jina) wakiwa safarini, gari walilokuwa wanatumia lilishambuliwa kwa risasi; na kwa bahati nzuri hakuna aliyepata madhara.

Kwa mujibu wa DCP Misime, polisi wanafuatilia tukio hilo kwa ukaribu sana, kwani uchunguzi ulishaanza baada ya kupokea taarifa, huku akisisitiza baada ya uchunguzi wa wataalam taarifa kamili itatolewa.



Mbunge wa Simanjiro, mkoani Manyara, Christopher Ole Sendeka (kulia) akizungumza na Mbunge wa Afrika Mashariki, James Ole Millya wakati wa mkutano wa hadhara jimboni humo juzi. Wa (pili kushoto) ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Simanjiro, Baraka Kanunga. **PICHA: GIFT THADEY**

# Majiji matano kufikiwa na mradi mabasi mwendokasi

**Na Mwandishi Wetu,**
TANGA

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), umetangaza kuja na mpango mpya wa kutoa huduma ya usafiri katika majiji ya Arusha, Tanga, Dodoma, Mbeya na Mwanza.

Mtendaji Mkuu wa DART, Dk. Athuman Kihamia, amesema serikali ina mpango wa kutoa huduma hiyo ya mabasi katika majiji yote nchini ili kukabiliana na msongamano wa watu na uhitaji wa mabasi hayo.

Dk. Kihamia alikuwa akizungumza katika Jiji la Tanga juzi, kuhusu mkataba wa miaka 12 itakaoingia wakati wowote mwezi huu; na Kampuni kutoka Falme za Kiarabu ya Emirates National Group (ENG) kwa ajili ya kuongeza wigo wa huduma za usafirishaji wa abiria jijini Dar es Salaam.

"Pia serikali ina mpango wa kutoa huduma hiyo ya mabasi katika majiji yote nchini, yakiwemo Mwanza, Arusha, Dodoma na Mbeya. Kwamba majiji ndiyo yenye msongamano wa watu; kwa hiyo yatapata huduma kama ilivyo katika Jiji la Dar es Salaam," alisema.


Kwa mujibu wa Dk. Kihamia, mchakato huo wa kumpata mtoa huduma bora nchini umekamilika na mtoa huduma huyo kutoka Abudhabi, ataanza kazi hiyo kwa kuongeza mabasi 177.

"Awamu itakuwa ni ya kutoka Mbagala kwenda Kivukoni, Mbagala/Gerezani na kwenda mpaka Morocco, na maeneo mengine ya mjini, ambapo miundombonu yake iko asilimia kama 98 hivi. Awamu hii itahitaji mabasi 755, mabasi yale makubwa yenye mita 18, mabasi 255 na mabasi yale ya wastani yenye mita 12, mabasi 500.

...Awamu ya tatu ni inayotoka Gongo la Mboto kwenda Gerezani, Gongo la Mboto kwenda Morocco, hadi Kivukoni na maeneo mengine ya mjini."

DART, ni taasisi ya serikali iliyoundwa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 120 la Mei 25, Mwaka 2007; chini ya Sheria Namba 30 ya Wakala za Serikali ya Mwaka 1997 na marekebisho yake.

Jukumu kuu la DART, ni kuanzisha na kuendesha mfumo wa usafiri wa mabasi yaendayo haraka kwa Jiji la Dar es Salaam.





# Wanaotorosha tumbaku kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi

**Na Halima Ikunjin,** TABORA

SERIKALI imesema kiongozi yoyote atakayebainika anajihusisha na utoroshaji na ulanguzi wa tumbaku atakufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi.

Hayo yalielezwa na Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Zakaria Mwansasu wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa 31 wa Chama Kikuu cha Ushirika cha WETCU mkoani hapa.

Alisema utoroshaji na ulanguzi huo unadhoofisha vyama vya msingi vya ushirika na kusababisha kufa kutokana na kudaiwa fedha nyingi na taasisi za fedha.

"Napenda kutumia fursa hii kuwaonya wale wanaohusika na utoroshaji na ulanguzi wa tumbaku kuacha mara moja kwani tumepanga kuimarisha ulinzi na watakaobainika watachukuliwa hatua za kisheria. Vitendo hivi vinaweza kukoma iwapo kila kiongozi na mwanachama watakuwa waadilifu kwa kufichua uozo huo" alisema Mwansasu.

Alisema kuwa tatizo ilo limechangia baadhi ya wakulima kukosa malipo yanayotokana na mauzo ya tumbaku, hivyo ni jukumu la viongozi wa vyama vya msingi vya ushirika kuwa wasimamizi wazuri na kufanya shughuli mbalimbali kwa uadilifu mkubwa, ili kupunguza malalamiko kwa wanachama.

Alisema endapo hali hiyo itajitokeza kwenye chama chochote msimu huu au wowote hatua kali za kisheria zitachukuliwa ili kukomesha mchezo huo mchafu katika zao la hilo.

Awali Mwenyekiti wa WETCU, Hamza Kitunga alisema mwaka huu chama hicho kupitia wanachama wake wanatarajia kupata kilo milioni 47 za tumbaku licha ya kuwepo na majanga yatokanayo na mvua za masika.

## Waamini waaswa kuwa makini na mitandao

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAAMINI wa Kanisa la TAG Ngokolo lililopo katika Manispaa ya Shinyanga, wameaswa kuwa makini na matumizi ya mitandao ya kijamii, hasa kuangalia mambo ya ovyo na kumsahau Mungu.

Kauli hiyo imetolewa na Meya wa Manispaa hiyo, Elias Masumbuko wakati wa maadhimisho ya miaka 85 ya kuanzishwa kwa Kanisa la TAG nchini.

Alisema ulimwengu wa utandawazi umekuwa ukiharibu watu wengi na hata kumsahau Mungu, hivyo wanapaswa kushika sana neno la Mungu na wasikubali kutawaliwa na mitandao ya kijamii kwa kuangalia mambo ya ovyo na kuingia kwenye ulimwengu wa shetani.

Aidha, Mchungaji kiongozi wa kanisa hilo, Christian Kubena, akizungumza wakati wa ibada alisema kufanya maadhimisho ni kufuata maandiko matakatifu ya Mungu ya kukumbuka na kuyaishi mambo mazuri ya watangulizi katika kuongoza kondoo wa Mungu.

Katibu wa Kanisa hilo, Gilselda Kasili alisema kuwa kanisa hilo limekuwa likitoa huduma za kiroho pamoja na kijamii kwa kushirikiana na taasisi isiyo ya kiserikali iitwayo Commpassion International, kuwahudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Alisema hadi sasa wameshahudumia watoto 250 kwa kuwapatia huduma za kiroho, kimwili na kiakili.




Waamini wa Kanisa la TAG Ngokolo, Manispaa ya Shinyanga wakiwa kwenye maandamano ya kuadhimisha miaka 85 ya kuanzishwa kwa kanisa hilo nchini, mjini Shinyanga jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Wachimbaji wadogo walia kuporwa maeneo na wawekezaji

**Na Remmy Moka,** SAUT

WACHIMBAJI wadogo wa madini katika mgodi wa makongolosi Kijiji cha Majimoto, Wilaya ya Serengeti mkoani Mara wamelalamika kuporwa maeneo na wawekezaji pasipo kulipwa fidia stahiki.

Wachimbaji hao walitoa malalamiko hayo wakati wa kikao baina ya wanakijiji na Mkurugenzi wa Shirika la Kutetea Haki za Binadamu la Lango la Matumaini Tanzania.

Nyigana Musa ni mmoja kati ya wachimbaji wadogo wa kijiji hicho alisema alishangaa kuona watu wakitumia eneo lake la uchimbaji pasipo makubaliano yoyote na kuambiwa kuachia eneo bila kulipwa fidia.

Hivyo aliiomba serikali kuwatazama kwa jicho la tatu ili kutatua tatizo ilo.

Aidha, aliutupia mzigo uongozi wa Serikali ya Kijiji Kwa kutochukua hatua zozote katika kuwasaidia wachimbaji hao.

Alisema baadhi ya maeneo wamiliki wamelipwa na mengine kutokulipwa sambamba na kunyang'anywa ubia wa kumiliki maeneo baada ya mwekezaji mzawa kuweka ubia na wawekezaji wa kigeni.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, Daud Charles alikiri uwepo wa malalamiko hayo na kusema baadhi ya wanachama hawajalipwa, huku baadhi yao wakiwa tayari wamelipwa.

Alisema lakini bado wanalalamika kutokulipwa jambo linalosababisha sintofahamu katika uongozi wa Kijiji, huku akidai baadhi ya wachimbaji kutokuwa waaminifu baada ya kulipwa .

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Lango la Matumaini Tanzania, Jackson Magesa aliiomba serikali kulichukulia suala hilo katika uzito ili kuondoa matatizo yanayowakabili wachimbaji hao na kuweka hali ya amani baina uongozi wa kijiji na wachimbaji.

Ofisa Madini wa Mkoa wa Mara, Amini Msuya alisema tatizo hilo linafanyiwa kazi na ofisi ya madini kwa kushirikiana na taasisi zingine.

# Walalamika kutozwa 100,000 kupata huduma ya uzazi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAJAWAZITO katika Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga waliojifungulia nyumbani wamelalamika kitendo cha kutozwa faini ya Sh.100,000 pindi wanapokwenda hospitalini kupata huduma ya uzazi.

Wamesema hatua hiyo imewasababisha wasiokuwa na uwezo kuendelea kukaa nyumbani pasipo kupata huduma ya kwanza wakiogopa gharama, huku wengine wakiendelea kuhatarisha usalama wao kwa kujiuguza kienyeji.

Walitoa malalamiko hayo wakati wa mkutano wa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita uliolenga kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi, hususani kwenye sekta ya afya, elimu, maji, kilimo na miundombinu ya barabara.

Mkazi wa Nyamilango, Richard Daudi, alisema kuwa wajawazito wengi wanajifungulia nyumbani ama njiani, wanapofika hospitalini kupata huduma ya kwanza wanatozwa kiasi hicho cha fedha.

Alisema wanapouliza sababu za kutozwa kiasi hicho wanahojiwa kwa nini wamejifungulia nyumbani badala ya vituo vya afya.

Mkazi mwingine kutoka Kijiji cha Mitonga, Elizabeth Paschal alisema wanapowapeleka hospitali watoto wenye umri chini ya miaka mitano kupata huduma wanatozwa fedha.

"Hivi Karibu Mkuu wa Wilaya nilimpeleka mtoto wangu hospitali alikuwa anaumwa na ana umri chini ya miaka mitano, kwenye mapokezi tu nilichajiwa Sh.5,000, nilikwenda kwa daktari hadi maabara nilipoelekea kwenye dirisha la dawa nilitozwa Sh.10,000 na nikapewa dawa za kutuliza maumivu tu sasa ile dhana ya kutibiwa bure iko wapi?"alihoji Elizabeth.

Aidha, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Ushetu, Dk. Alphonce Malunde alisema, siyo halali wananchi au mgonjwa hasa wajawazito kutozwa fedha kwa kile kinachodaiwa ni faini kwa kujifungulia nyumbani.

Alisema badala yake anapofika hospitalini anatakiwa kuelimishwa juu ya umuhimu wa kujifungua kwenye kituo cha afya ili kulinda usalama wake na mtoto.

Alisema miongozo na sera ya serikali ni kwamba watoto chini ya umri wa miaka mitano wanapaswa kupata huduma za matibabu bure na kama mgonjwa ataombwa fedha anatakiwa kupewa ufafanuzi ni huduma gani amelipia.

Hivyo, aliwataka wagonjwa pindi watakapoombwa fedha wafike ofisni kwake au Ofisi ya Mganga Mfawidhi kutoa taarifa.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Hadija Kabojela aliwashauri wajawazito kuhudhuria kliniki vipindi vyote, ikiwa pamoja na kujifungulia kwenye vituo vya afya.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita aliwakemea watumishi wa afya ambao wamekuwa na lugha mbaya kwa wagonjwa hasa wajawazito wanaofika vituoni kujifungua.

Alisema watakaobainika wanaendeleza tabia hiyo watawajibishwa kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma kwani wanasababisha wajawazito kukimbia kliniki na kujifungulia majumbani.



Ukurasa 12

UTAWALA BORA KAZINI...

**Dk. Biteko alipoibua njia ya ufanisi na mafanikio katika sekta nishati**



Ukurasa 13

**KIKUNDI MAARIFA KC...**

Kinamama wanaobadili shida zao hadi mapinduzi maendeleo


# siasa

JUMATANO APRILI 3, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**Mbowe anapoingia katika orodha watekelezaji makubwa siasa nchini**

# Siku Dk. Samia alipotua kikaoni AU, akiwa na Diplomasia Uchumi mkononi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, katika staili yake kimataifa, amekuwa na ziara nyingi nje ya nchi ikiwa ni sehemu ya kuboresha diplomasia kimataifa, ambayo inaendana sasa na Diplomasia Uchumi.

Mnamo Februari 17 mwaka jana, pia akawa na ziara kuhudhuria mkutano Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi za Afrika Mashariki (EAC) uliofanyika katika Jengo la Usalama na Amani la Julius Nyerere, lililopo katika Makao Makuu ya Umoja wa Afrika (AU) Addis Ababa nchini Ethiopia.

Ni sehemu ya kuhudhuria namna yake, hasa katika rekodi yake na heshima ya Tanzania katika chombo hicho kisichoweza kutenganishwa na mwasisi wa taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Ni mkutano uliofuatiwa na Mkutano wa Baraza la Amani na Usalama (PSC) la Umoja wa Afrika (AU) pamoja na wakuu wa nchi na serikali wa Afrika kujadili hali ya usalama katika eneo la Mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), chini ya Mwenyekiti wake Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa Februari,17 2023.

Siku iliyofuata, Rais Samia akatoa hotuba ya kujitambulisha katika mkutano huo wa 36 wa Umoja wa Afrika (AU) uliofanyika katika Ukumbi wa Nelson Mandela, kwenye makao makuu ya Umoja huo.

Rais Dk. Samia akasema, alikuwa na jukumu la kulileta taifa pamoja na kujipanga upya kuendeleza masuala yalioachwa na mtangulizi wake aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Rais John Pombe Magufuli, ambaye sasa ana miaka mitatu tangu kifo chake.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Rais wa Somalia Hassan Shekhe Mohamud, katika ukumbi wa Nelson Mandela, makao makuu ya Umoja wa Afrika (AU) jijini Addis Ababa, Ethiopia, Februari 18, mwaka jana. **PICHA: MAKTABA**

Rais Dk. Samia akasema, katika kipindi cha miaka miwili amekutana na wadau wa siasa wa ndani ya nchi na makundi mbalimbali ili kuliweka taifa pamoja.

Vile vile, Rais Samia akaambia namna amewahakikishia kuwa Tanzania itaendeleza misingi ile ile ya Sera ya Mambo ya Nje iliyowekwa na waasisi wa taifa (ikiwamo Diplomasia Uchumi).

Rais Samia akatumia fursa hiyo, kuwashukuru na kuwapongeza wakuu wa nchi na serikali kwa kupitisha azimio la kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya AU, ambayo imemuwezesha siku hiyo kuhutubia Mkutano huo kwa lugha hiyo.

Vilevile, naye akawaalika wakuu wa nchi na serikali katika Mkutano wa Kilele cha Jukwaa la Kijani lililofanyika siku tano kuanzia Septemba 4 hadi 8, mwaka jana

Rais Dk.Samia, mpenzi wa kilimo, akaeleza namna masuala ya mifumo ya chakula barani Afrika ,kwa kushirikiana na wakulima, wafanyabiashara na wadau mbalimbali kutoka nchi za Afrika na nje ya Bara la Afrika.

Mbali na kushiriki mkutano huo, Rais Dk. Samia akakutana na kuzungumza na viongozi wa taasisi mbalimbali, wakiwamo Waziri Mkuu wa Ethiopia Dk. Abiy Ahmed na Rais wa Zambia Hakainde Hichilema.

Pia, wamo Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi ya Kundi la Mashirika ya Ndege ya Ethiopia, Girma Wake na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia anayeshughulikia Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika Bi. Victoria Kwakwa.

Rais Dk, Samia amekuwa akiamini katika kujenga na kudumisha mahusiano ya kidiplomasia na mataifa na jumuia zingine.

Amekuwa akifanya vikao vingi na kukutana na viongozi mbalimbali wa mataifa ya Afrika na nje ya Afrika pamoja na mashirika ya kimataifa katika safari zake kuboresha mahitaji ya uchumi nchini.

# Dk. Biteko alipoibua njia ya ufanisi na mafanikio katika sekta nishati

**Na Dk. Reubeni Lumbagala**

"TUNAFANYA haya katika kusaidia wananchi kero zao mbalimbali ili tutakapokufa watu wasitutafute kwenye makaburi yaliyonakshiwa na marumaru, bali kwenye mioyo ya wale ambao walinufaika na sisi kutokana na haya tunayoyafanya."

Maneno hayo maarufu yaliwahi kusemwa na mfanyabiashara na kiongozi mashuhuri wa zamani wa Morocco, Abu Abdullah Muhammad Ibn Battutah. Hiyo kwa mbali, inafanana na kauli aliyoitoa wakati fulani Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi kwamba 'Maisha ni historia tu, basi jitahidi uwe historia nzuri."

Swali libaki kwa kiongozi katika ofisi ya umma, anadhani kutokana na utumishi wake, hata kabla hajaondoka duniani, itakuwa historia nzuri? Atagusa mioyo ya watu watakaokuwa wanakumbuka utumishi wake uliotukuka?

Chama cha TANU (Tanganyika African National Union) kilichofanya kazi kubwa ya kuleta ukombozi Tanganyika (sasa Tanzania Bara), kiliweka ahadi zake ambazo wanachama na viongozi wake wa wakati huo na sasa CCM wanapaswa kuzielewa, kuziishi na kuzitendea.

Mathalani, moja ya ahadi za mwanachama wake ni isemayo: "Cheo ni dhamana, sitatumia cheo changu wala cha mtu mwingine kwa faida yangu."

Kimsingi, ahadi hiyo inalenga kuwakumbusha watumishi, watendaji na viongozi kuwa nafasi walizo nazo si zao, wala za kudumu, bali ni utumishi wa umma kwa muda tu, hivyo wanawajibika kuwatumikia wananchi kwa ufanisi. Msisitizo wake hapo ni kwamba, haja ya kupeana dhamana na kamwe wasitumie nafasi zao au za watu wengine, kwa manufaa yao binafsi pekee.

Licha ya kuwa ahadi hiyo ni ya wanachama CCM, lakini anaitaja inapaswa kufanyiwa kazi na yeyote anayekabidhiwa ofisi ya umma.

Kwa mtumishi au kiongozi anayelewa vyema ahadi hiyo na kuifanyia kazi kikamilifu, utumishi wake unaleta manufaa na faida nyingi kwa wananchi na taifa na daima atakumbukwa na kizazi cha sasa na kijacho.

Kuishi katika ahadi hiyo inatakwa ni kuwatumikia wananchi kwa kuhakikisha maslahi na haki zao wanazipata kwa wakati na kamwe hatakuwa sehemu ya kukwamisha na kuzuia kabisa haki kupatikana bali kuiwezesha kupatikana.

Siku chache zilizopita, akasikika Sheikh mmojawapo akiwaambiwa waumini wa dini yake wanaoendelea na mfungo, akisema kwamba muumini anayemfurahisha sana Mwenyezi Mungu, ni yule ambaye watu wengi wananufaika naye.

Kwamba unavyopendwa na Mungu, kadri watu wengi wanavyonufaika naye, ndivyo pia anakuwa Jirani na baraka za hapa duniani na maiosja ya baadaye.



Zilivyo pilika na ugeni wa wakaguzi, katika ukamilishaji mradi wa umeme, Bwawa la Julius Nyerere. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

> "Hivi vyeo vyote mlivyo navyo, kikiwamo cha kwangu sio vya kwetu ni 'temporary' (vya muda mfupi) kwa ajili ya 'ku-service' (kuhudumia) wakati ule. Kwanini msijifanyie marafiki kwa vyeo mlivyo navyo?



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dotto Biteko.

### NAIBU WAZIRI MKUU

Ni katika hilo, ndipo anapongezwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, ambaye kila mara amekuwa akisisitiza uwajibikaji, uzalendo na moyo wa dhati wa kuwatumikia wananchi, kwani kwa kufanya hivyo, kero za wananchi zinatatuliwa.

Vilevile ukatajwa ni mustakabli wa kufikiwa mipango na malengo ya nchi unatimia kwa wakati. Mathalani, hivi karibuni Dk. Biteko akifungua Mkutano wa Tano wa Baraza la Wafanyakazi la Wizara ya Nishati, akaisisitiza kuwa cheo ni dhamana, hivyo watumishi wa Wizara ya Nishati wakiwamo Tanesco wawahudumie wananchi, ili nchi iweze kusonga mbele kimaendeleo.

"Yaani wewe kuwa mtu wa Tanesco au kuwa mtu wa Wizara ya Nishati, unaonaje fahari kuabudiwa na kutukuzwa kwa sababu ya cheo ambacho kwanza sio chako, ni cha watu...

"Hivi vyeo vyote mlivyo navyo, kikiwaemo cha kwangu sio vya kwetu ni 'temporary' (vya muda mfupi) kwa ajili ya 'ku-service' (kuhudumia) wakati ule. Kwanini msijifanyie marafiki kwa vyeo mlivyo navyo?

"Kwanini mnajitengenezea maadui kwa vyeo mlivyonavyo? Unafanya Tanesco ambalo ni shirika zuri la nchi linaonekana ni shirika ambalo ni baya la hovyo. Akisimama mtu wa Tanesco mahali popote, watu wanaanza kucheka utafikiri kasimama 'comedian' (mchekeshaji), kwa nini?

'Ni kwa sababu ya 'character' (tabia) za watu wa mle ndani. "Kumpelekea mtu nguzo mpaka akupe hela, na wananchi wapo wanaojua kushawishi.

"Atakushawishi kwa haraka zake anakwambia, 'bwana nisaidie niwekee nguzo hapa haraka kuna milioni hapa.'

"Siku nguzo imesimama atakumbuka milioni yake na atakwenda kwa wengine kuwaambia wale jamaa hawapeleki nguzo mpaka milioni, unahangaika hapa, mimi nilivyomgonga milioni, mbona kesho yake ilifika. Tunaonekana wote humu wapiga dili," anasema.

Hapo anatoa rai kwamba, viongozi wote wanaochaguliwa au kuteuliwa, wana jukumu la kuwatumikia wananchi wanaowaongoza na kuhakikisha nafasi walizo nazo zinakuwa daraja la kufanikisha maendeleo badala ya kukwamisha.

Pia, anahimzia kuwapo wanaoelewa vyema dhana ya 'cheo ni dhamana', hivyo kwa wakati walionao wa kuwatumikia wananchi, wanatimiza wajibu wao kikamilifu na kwa moyo wa uwajibikaji na uzalendo mkubwa.

Anatumia methalli na usemi; "cheo ni kama koti la kuazima ambalo kwa kuwa lieazimwa, ni lazima likarudishwa kwa wenyewe. Hivyo, lahitaji unyenyekevu katika kuwatumikia wananchi."

Eneo jingine analolitaja Dk. Biteko, ni kuwapo baadhi watu ambao kwao cheo ni fimbo ya kuwachapa wengine, hivyo anawataka kuuonyesha umuhimu wa nafasi zao kuwakwamisha wengine.

Anakumbusha kuwa, viongozi wanaotumia nafasi zao kuwaumiza wengine wanapaswa kubadilika, kwani cheo ni dhamana.

Vilevile anasema kwa watumishi wa umma waliopewa dhamana kuwatumikia wananchi, wapo wanaowajibika, pia wapo wanaokwamisha wengine kwa nafasi walizonazo.

Ni nafasi inakumbusha mshahara wanaolipwa viongozi wanavyofurahia, hata usafiri wanatumia (kama upo), vinatokana na kodi za wananchi wanaovuja jasho kuwatumikia.

Kimsingi, anawachambua waajiri wao halisi, kuwa ni wa wananchi na si watu kusukumwa, bali wanatakiwa wautumikie umma. Kwa lugha nyingine, ni ufafanuzi kwamba walioko kwenye ofisi za umma wajue wao ndio watumwa wa wananchi na si kufikiri kwamba wananchi wanapaswa kuwatumikia wao.

Biteko alipokuwa Waziri wa Madini, alishawakumbusha wakurugenzi ndani ya wizara hiyo kuacha kuwanyima magari watumishi wa ngazi za chini pindi wanapokuwa na ziara za kikazi, bali magari husika wayatumie kwa wakati kufanakisha kazi ya msingi, wasikwamishe maendeleo.

Inakumbuishwa mara zote, huduma bora kwa wananchi ni mkazo unaohimizwa na Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi mahiri wa Dk. Samia Suluhu Hassan.

***• Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma. Kwa maoni, piga simu: +255 620 800 462.***

KIKUNDI MAARIFA KC....

# Kinamama wanaobadili shida zao hadi mapinduzi maendeleo

Na Zanura Mollei

- Darasa la TGNP yatumika silaha kudumu
- Mageuzi; waliojiuza ngono, dereva bajaji...



Sehemu ya Ofisi ya Mtaa wa Saranga, Kimara, Dar es Salaam, kliniki ya mtoto na mjamzito inaendeshwa chini ya mti. Kikundi cha kinamama sasa kinafanyia mageuzi. **PICHA: MAKTABA**

HADI sasa unatajwa, utawala bora unafanikiwa kubadili maisha ya Wakazi wa kata ya Saranga, baada ya kugeuza changamoto zao kuwa fursa kwao.

Kilichoko, wananchi wengi wamekuwa wakiamini maendeleo katika jamii yanapaswa kutekelezwa na serikali pekee, lakini wakazi wa kata hiyo sasa wanasema 'hapana, maendeleo ni jambo la kila mmoja katika kuhakikisha taifa linapiga hatua.'

Sasa, wanatafuta njia ya kukabiliana na matatizo mbalimbali ikiwamo changamoto za miundombinu ya afya, elimu, pamoja na kujengeana uwezo kuinuana kiuchumi kama jamii.

Maria Mwigune, Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa (KC) Kata ya Saranga Jimbo la Kibamba Wilayani Ubungo, anaisimulia Nipashe chanzo cha kituo hicho kuleta mageuzi ya kijamii na kubadili maisha ya mtu mmoja mmoja.

Anasema kuwapo changamoto ya maji katika Shule ya Msingi, Kimara 'B', Dar es Salaam, imewafanya wanafunzi wengi kusitisha safari ya kukosa maji na wakaugua maradhi ya UTI.

Ni hali iliyowakutanisha wazazi katika shule hiyo kujadili majibu ya kutatua tatizo hilo na kukaibuka mvutano wa wazazi kuchanga, lakini waraka wa elimu kwa wakati huo ulikataza michango kwa wanafunzi.

"Katika hili Mwalimu mkuu hakutuunga mkono kwa kuhofia kutokutii agizo la serikali," anaeleza Mwigune na kuongeza:

"Nilivyoona kuna mvutano nikawaeleza wazazi wezangu anayetaka tuchange kwa ajili ya watoto wetu waweze kupata huduma katika mazingira salama wajitokeze, wakajitokeza wanawake 16.

Wazazi walijichanga wakipokea wazo na ndani ya wiki moja, wakafanikiwa kukusanya Sh. milioni 1.3, walizokarabatia kisima na kununua mota mpya, maji yakaanza kupatikana shuleni, ni kipindi kulikuwapo mlipuko wa ugonjwa UVIKO 19.

Anasimulia siku moja alipigiwa simu kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) wakimtaka kuhudhuria mafunzo na kikundi chake, wakaenda. Baada ya kupata elimu ya kubadilisha changamoto kuwa fursa, wakarejea kutoa elimu kwa makundi mengine, kutatua changamoto zao kijamii.

"TNGP walivutiwa na namna tulivyoweza kuelimisha na kushawishi jamii kutatua matatizo kwa kushirikiana, ndipo wakatuita kwenye mafunzo, tunawashukuru..." anasema Maria.

Maria anasimulia changamoto ziliibuliwa nyingi katika maeneno mbalimbali, Mtaa wa Saranga waliibua tatizo la ukosefu wa zahanati, inayowaumiza wajawazito wake, kufanyiwa vipimo katika Ofisi ya Kitongoji kipindi cha kliniki, wakiwa chini ya mti.

"Kama jamii tuliweka mpango wa haraka wa kuanza kukusanya michango kwa ajili ya ujenzi wa zahanati.

"Tulifanya hivyo kwa kuwa mazingira ya huduma ya afya yalikuwa hatarishi, kumpimia mtoto uzito kwa kumning'iniza kwenye miti...kinamama wakati wa kujifungua unapofika wanapelekwa Kituo cha afya Kimara," anaeleza Maria.

Anasimulia kinamama walichanga fedha za ujenzi na mwaka 2022, mkakati kujenga zahanati ulianza, huku mbunge wa jimbo akiahidi kuchangiam kuunga mkono jitihada zao, ikkiwa ni zao la elimu waliopata, changamoto kuhamishiwa mtazamowa maendeleo.

"Ujenzi wa zahanati unaendelea, ila bado watoto wanapatiwa huduma ya vipimo kwa kuning'inizwa kwenye mti na wanawake bado wanafanyiwa vipimo kwa ajili ya kliniki kwenye ofisi ya mtaa" anasema.

Anataja shida nyingine inatyowakabili ni usumbufu waliopata kwa wasafirishaji (Bajaji) kukosa maegesho rasmi, hawakutambulika na kuna wakati wakatozwa fedha ambazo hazikujulikana zinakoenda.

'Kama kituo tulibeba changamoto ile na kuwashauri njia sahihi ya kuweza kufanya shughuli zao ni kujisajili ili waweze kutambulika kisheria pamoja na kuhakikisha wanapatiwa eneo maalum." Anasema na kuendelea;

### WAKABILI UHALIFU

Hadi sasam, anasema kituo kimefanikiwa kudhibiti matukio ya kihalifu yaliyotokea katika eneo lililotambulika kwa jina maarufu "Chenji Hairudi"mtaa wa Stopover, ambayo yalihusisha biashara ya uuzaji mwili, ubakaji, wizi na uuzwaji wa pombe haramu.

Anasema kikundi chao kilimamua kuzungumza nao wakaeleza changamoto zao, hususani wafanyabiashara wakubwa, pia Mama Lishe namna ya kujikomboa kupitia mikopo sahihi na siyo 'mikopo ya kausha damu', hata wakajitenga na biashara ya uuzaji mwili.

Maria akasumilia: "Si lazima kuuza mwili ndio upate fedha ya kujikimu kimaisha. Tuliwafanyia vipimo vya afya na katika kukabiliana na mikopo kausha damu. tuliwajengea uwezo....

"Wamebadilika! Wana kikundi chao kinaitwa Elimika kina jumla ya watu 49, wanafanyabiashara kwa utulivu, amani wamegeuka kuwa walinzi na kuzuia biashara ya ngono."

Kwa mujibu wa Maria, eneo la ngono nalio limebadilika jina kutoka 'Chenji hairudi,' hadi sasa inaitwa Maendeleo.

> Hakuna mtu anayewaingilia katika utekelezaji wa majukumu yao, wanafanyakazi yao vizuri na wapo imara tunawashukuru....

### MAZINGIRA

Vilevile hatua ikachukuliwa katika kumkwamua mwanamke na kijana kiuchumi, Maria anasema walipoona kata hiyo iko juu kuchafua mazingira, wao kikundi cha Taarifa na Maarifa, wakageuza hilo kuwa fursa kwa kutengeneza mbolea, inayotumika sasa kuzalisha mboga na kuotesha maua.

"Tulifanikiwa kupata mkulima wa pilipili kutoka mkoa wa Singida tulimuuzia ametupatia mrejesho kuwa mbolea hiyo inafaa pia katika kilimo hicho," anasema.

### DEREVA BAJAJI

Longlinus Haule, ni dereva Bajaji katika kata ya Songara, anayesema walikuwa wakipitia changamoto ya usumbufu wa eneo la kupaki kwa shughuli zao, lakini baada ya kupatiwa elimu na uongozi wa kituo hicho, sasa utulivu umetawala kazi zao.

Anasema kikundi chao kina madereva 80, kimesajiliwa, kinatambulika kwa jina la Kumbajo. Awali walipatikana Mtaa wa Upendo na sasa wapo Kimara Stopover.

### MWENYEKITI UWT/DIWANI

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi(UWT) Mtaa wa Stopover, Habiba Magero, anasema matukio ya kihalifu katika kata hiyo yamepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na jitihada zinazofanywa na kituo hicho cha kinamama.

Diwani wa Kata ya Saranga, Edward Laizer, anasema kata hiyo ina jumla ya wakazi zaidi ya 143,000 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi Mwaka 2022.

Anaeleza kuwa kituo cha taarifa na maarifa kilitambulishwa kwake na asasi ya TGNP, akinena: "Kituo hiki kimekuwa mkombozi katika kata hii kwa kusaidiana na serikali kutatua matatizo na kudhibiti uhalifu".

Anasema Mtaa wa Saranga wananchi walichanga shilingi milioni 22 kujenga zahanati na mbunge wa jimbo hilo, Issa Mtemvu, kupitia mfuko wa jimbo alitoa shilingi million 10 kwa ajili ya kuongeza majengo na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kupitia makusanyo ya ndani kwa bajeti ya fedha mwaka uliopo, 2024/25, imetenga shilingio million 50 kusogeza ujenzi huo.

"Kata hii inawakazi wengi sana ndio sababu maendeleo yanakwenda taratibu, tumezungumza na TANROAD waweze kutupatia eneo la wazi ambalo linaonekana kuwa msitu na wahalifu hujificha humo," anasema lazier.

Anataja lengo ni kuwekwa vibanda wafanyabiashara (machinga) na wamekubali kujenga vibanda 950 na wananchi watachangia kodi za kuvitumia.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Mbowe anapoingia katika orodha watekelezaji makubwa siasa nchini

**Na Sabato Kasika**



Mweyekiti wa CHADEMA, Freman Mbowe (mbele katikati), akiwa katika maandamano ya chama chake. **PICHA: MAKTABA**

IKO wazi hadi sasa kinapotajwa chama kikuu cha upinzani katika sura ndani na nje ya Bunge, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ndicho kinashika nafasi hiyo.

Swali linapokuja sababu za msingi, kinajijulisha katika idadi ya wanachama wake, hata wabunge ambao kilikuwa nao kwenye ulingo wa bunge kabla hakijakumbwa na changamoto.

Kwa sasa mshindani kisiasa anayeitoa jasho CCM pale wanapochuana katika ubishani wa kisiasa, nje ya sanduku la kura, bado CHADEMA inashika nafasi hiyo.

Pale unapochimbwa mzizi wa uimara huo, hapo nafasi ya mwenyekiti wake wa sasa, Freeman Mbowe inaonekana. Pia, inapoaanza safari ya chama hicho tangu zama hizo katika uasisi wake, leo ikiwa miaka 30 na ushee, wengi waliitafsiri CHADEMA kama 'chama cha wakubwa' kwa maana ya wale wenye uchumi mzuri.

Pia, ikasambaa chama hicho kimeegemea sana ufuasi wa Kanda ya Kaskazini kwenye uasisi wake mwaka 1992, ishara yake ikienezwa chama cha matajiri, pia unasaba wake kimeegemea Kanda ya Kaskazini, kilipozinduliwa Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Waziri wa Fedha Mstaafu, Mzee Edwin Mtei ndiye Mwenyekiti wa kwanza taifa wa chama hicho tangu mwaka 1992 hadi 1998, akiwa mwanachama mwenye kadi namba moja.

Kadi namba mbili ikashikiliwa na Brown Ngwilulupi (marehemu), aliyewahi kuwa Meneja Mkuu wa Kiwanda cha Sigara (TCC).

Mwanasheria na Naibu Gavana Mstafau wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Bob Makani (marehemu) aliyemrithi Mtei tangu 1998 hadi 2004, kuiongoza alikuwa na kadi namba tatu. Kwa kuwa aliwahi kuwa Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika, alivuta wanasheria wengi CHADEMA.

Baada ya Mzee Makani kumaliza muda wake, Mbowe alichaguliwa kuwa mwenyekiti wa chama hicho taifa na kila uchaguzi amekuwa akishinda na kujikuta akiendelea kushikilia nafasi hiyo hadi sasa.

Lakini, nikirudi nyuma kwanza, Mbowe ni nani? Huyu ametoka katika nyumba inayohubiri siasa, baba yake mzee Aikaeli Mbowe alikuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya TANU kisha CCM.

Hivyo, ni wazi Mbowe (mtoto), anaijua siasa, ndio maana akatumia mageuzi ya kisiasa kwenda upande wa pili kama walivyofanya baadhi ya watoto wa waasisi wa TANU akiwamo, Makongoro Nyerere.

Mbowe huyo huyo, ndiye aliyebadili upepo wa CHADEMA na kusababisha chama kuwa na wafuasi wengi, na kuondoa dhana iliyojengeka kuwa ni chama cha matajiri au Kanda ya Kaskazini, kumfuata Mtei.

Tangu ashike nafasi hiyo, amekitoa chama kuwa cha watu wa chache kuwa cha wengi, hivyo ni wazi kwamba inaweza kuwa vigumu kumtenganisha Mbowe na kuzaliwa kwa CHADEMA.

### WAKATI MGUMU

Mbowe anashika nafasi hiyo, wakati wa migongano na migogoro ndani ya vyama vya upinzani vikiwamo vya NCCR-Mageuzi, UMD na vingine vingi vilivyokumbwa na kadhia hiyo kubwa.

Lakini kinyume chake, ametumia fursa hiyo kuondoa kwamba chama hicho ni cha vigogo na kukileta kwa wengi, wakajiunga nacho kwa kukiona kuwa ndicho chama chenye upinzani wa kweli.

CCM imewahi kusema kuwa inategemea kura za wanawake kwamba ndio mtaji wao, lakini kwa upande wa Mbowe, akajikita katika vyuo na kuchota wasomi wakiwamo kina Zitto Kabwe, Kalisti Komu na wengine wengi akatengeneza ngoma kubwa.

CHADEMA kimewalea na kuwafikisha hapo walipo, vilevile chini ya uongozi wa Mbowe, kimeonyesha ndicho chama imara huku vingine vikikumbwa na migogoro, kuchoka au kusambaratika na kusababisha baadhi ya wanachama kwenda CCM.

Ndani ya wakati huo, chama hicho kilikuwa kimeshaweka idadi kubwa ya wabunge, nahodha wao akiwa Mbowe Hai, lakini baadaye walipata misukosuko hadi kukosa ubunge, lakini Mbowe ameendelea kuwa imara na kuweka msukumo wa siasa za CHADEMA.

Aidha, ni kipindi hicho CCM nayo ikawa makini na kuwekeza katika vyuo ikianzia Chuo cha Mzumbe kama ngome yake kuu wakapatikana vijana wakiwamo Dk. Emmanuel Nchimbi ambaye kwa sasa ni Katibu Mkuu wa chama hicho, Amos Makalla na wengine wengi.

Pia, kama ilivyo kwa vyama vya siasa, CHADEMA nayo imewahi kupitia magumu wakati fulani kati ya mwenyekiti Mbowe na makamu wake Chacha Wangwe (marehemu).

Ulitokea mpasuko, moja ya safu yake muhimu, kijana aliyekwisha iva kisiasa Zitto Kabwe mpinzani wa CCM na Profesa Kitila Mkumbo wakaondoka huku Prof. Mkumbo akienda CCM.

Yupo Joseph Selasini aliyejiunga baadaye na chama hicho na kuwa mbunge wa Rombo mkoani Kilimanjaro, lakini naye akaondoka kwenda akiwa na Kalisti Komu wakaenda NCCR- Mageuzi.

Hivyo, magumu yaliyoikumbuka kambi ya upinzani huwezi kuyatenganisha na Mbowe ambaye ni mwathirika mkuu, ambaye amewahi kuwekwa ndani miezi sita bila dhamana.

Ni katika kipindi hicho chote hata kufikia siasa za Tanzania katika siasa za kimataifa, msamiati Mbowe unachukua nafasi.

### 4R ZA RAIS SAMIA

Itakumbukwa kuwa mwanzo wa awamu ya sita na siasa zake za 4R, utekelezaji wake ulimhusu Mbowe moja kwa moja, kwani siku aliopata msamaha, akawa na mwaliko wa kuteta jambo lao na mkuu wa nchi.

> R ya kwanza ambayo ni 'Reconciliation', yaani maridhiano au upatanisho, R ya pili ni Resilience', yaani ustahimilivu, R ya tatu 'Reforms', yaani mageuzi na R ya nne ni 'Rebuild', yaani kujenga taifa.

R ya kwanza ambayo ni 'Reconciliation', yaani maridhiano au upatanisho, R ya pili ni Resilience', yaani ustahimilivu, R ya tatu 'Reforms', yaani mageuzi na R ya nne ni 'Rebuild', yaani kujenga taifa.

Falsafa hiyo yenye 4R inagusa kila nyanja, sasa imepita miaka miwili hatujasikia Mbowe akilalamika wala kulaumu haki yake. Hapo historia yake ndefu na hulka vinatoa ishara kuwa 'roll model' wake ni mzee Nelson Maendela, Rais kwanza mweusi wa Afrika Kusini.

Mzee huyo anasimama katika utashi wake huo licha ya kukaa kwa miongo miwili na ushee gerezani. Hivyo, kikubwa ndani ya utashi wake, daima Mbowe naye hajatoka ndani ya mstari wa anachodai ndani ya siasa za CHADEMA. Mathalani, simulizi za katiba na haki za Watanzania.

Huku chama hicho kikidumu nje ya mipasuko inayoviathiri vyama vya upinzani, kimekuwa na nguvu thabiti ambayo hakuna wa kukishangaa kwa jinsi kinavyojitanabaisha.

Mfano, maandamano ya chama hicho yametekelezwa katika majiji manne nchini, huku yakifana. Hapana shaka Freeman Aikael Mbowe anaingia katika orodha ya viongozi bora wa kisiasa nchini.

Kwanini? Kwa sababu hajawahi kukaa nje ya msimamo wake anaoamini, hulka yake ni chanda na pete ya hayati Nelson Mandela, ambaye hakukata tamaa kupambana hadi nchi yake ilipopata uhuru.



## Daktari bingwa aonya ulaji vyakula wanga, chumvi, mafuta

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

DAKTARI Bingwa wa magonjwa ya ndani kutoka Hospitali ya St. Camillus jijini Dodoma Dk. Bonaventura Mpondo amesema jamii inapaswa kuzingatia kupunguza vyakula vyenye wanga, chumvi na mafuta ili kujilinda na magonjwa ya moyo, shinikizo la damu na kisukari.

Amesema mtu ambaye anatumia vitu hivyo hupelekea hatari ya kupatwa na tatizo la figo.

Dk. Mpondo alisema hayo juzi jijini Dodoma wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuongezeka kwa wagonjwa wa figo nchini.

Dk. Mpondo alisema takwimu zinaonesha kuwa magonjwa ya moyo, shinikizo la damu na kisukari ndiyo yanayoongoza kwa kusababisha tatizo la figo ambapo ameiasa jamii kupima afya zao mara kwa mara ili kutambua magonjwa hayo mapema.

Aidha, alishauri jamii kufuata masharti ya kitaalamu juu ya matumizi sahihi ya dawa kwa wale wanaogundulika kuwa na magonjwa hayo pamoja na matibabu yasiyo ya dawa ambayo ni mtindo bora wa maisha ili kuzilinda figo zao.

Aliongeza kuwa mgonjwa wa figo anapaswa kutokata tamaa akisema zipo njia za kitaalam kumsaidia ikiwemo matumizi ya dawa, ushauri wa mpangilio wa lishe usafishaji wa damu au kupandikiza figo pale inapobidi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kati ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika, aliwataka wananchi kuzingatia mtindo bora wa kula kwenye maisha yao ili kulinda figo zao.

Dk. Chandika, alisema wananchi wanapaswa kufanya mazoezi pamoja na kuzingatia mlo usioathiri moyo ili kuzilinda figo.

"Mtindo bora wa maisha unaozingatia milo isiyoathiri moyo utaisaidia kuzilinda figo," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya BMH.

Dk. Chandika alisema wagonjwa 50 wenye tatizo la figo husafisha damu kwa siku katika kKitengo cha kusafisha damu katika idara ya magonjwa ya figo katika Hospitali ya BMH.

Alisema watu wenye tatizo la figo wanasafisha damu mara tatu kwa wiki.

Dk. Chandika alisema mpaka sasa, BMH imeshafanya oparesheni za upandikizaji figo kwa watu 36 tangu huduma hii ianze miaka sita iliyopita.

# Serikali yatoa bil.3/- utekelezaji mradi wa umwagiliaji Iramba

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IRAMBA

SERIKALI imeipatia Wilaya ya Iramba mkoani Singida Sh.bilioni tatu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa umwagiliaji mashamba uliopo katika Bonde la Wembere.

Katika mradi huo zaidi ya hekari 36,000, zimetengwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Urughu kwenye mkutano wa hadhara wa mbunge wa Iramba Magharibi, Dk. Mwigulu Nchemba.

Mwenda alisema utekelezaji huo ni agizo lililotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan la kutaka yachaguliwe maeneo ya kuanzisha kilimo cha umwagiliaji ili kuhakikisha usalama wa chakula na kilimo.

"Mradi huu utakapokamilika utawafanya wananchi walime wakati wote wa kiangazi na masika kwa sababu watakua wana uwezo wa kuhifadhi maji, tayari wataalam na maofisa wa umwagiliaji wameshafika kujitambulisha ofisini kwangu," alisema.

Dk. Nchemba ambaye pia ni Waziri wa Fedha, aliwaomba wananchi kuendelea kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kwa sababu anaendelea kufanya makubwa yanayoboresha ustawi na kujali afya zao.

Alisema fedha zinazoletwa Wilaya ya Iramba na maeneo mengine nchini zinakwenda kujenga miradi mbalimbali ya maendeleo, vikiwemo vituo vya afya katika kila tarafa na maeneo muhimu.

"Anajali afya yako anakupa mtaji wa kufanya kazi kwa sababu anaweza kuwa na mipango mizuri ya kazi lakini asipokua na afya njema hawezi kuitekeleza mipango hiyo," alisema.

Aliongeza kuwa: "Mama ametafsiri kwa vitendo kauli ya kuwapenda Watanzania na anashughulikia tatizo la ugumu wa maisha kwa kupeleka miradi mikubwa ya umwagiliaji hata ngazi ya kijiji ambayo inatoa majawabu".

Dk. Mwigulu alisema anaorodha ya matatizo na kutoa majawabu kivitendo kwa sababu nchi nzima kuna miradi ya umwagiliaji na miradi ya kufungua barabara ambapo itabadilisha maisha ya Watanzania kutoka katika ugumu.



Baadhi ya Wabunge wakiwasili katika viwanja vya Bunge, kwa ajili ya kushiriki kikao cha kwanza cha mkutano wa 15, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Profesa SUA afanya utafiti unenepeshaji ng'ombe

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MTAFITI na Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Prof. Sebastiani Chenyambuga, amefanya utafiti wa unenepeshaji wa ng'ombe, ili kusaidia uzalishaji wa nyama ya ng'ombe wa kienyeji katika Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

Akizungumza na waandishi wa habari, Prof. Chenyambuga alisema mradi huo wameshirikiana na wakulima wa Kijiji cha Mtanana A na B, lengo kuu likiwa ni kuboresha uzalishaji wa nyama zitokanazo na ng'ombe wa kienyeji.

Alisema utafiti alioufanya utasaidia nyama za ng'ombe zinazozalishwa nchini kupelekwa katika soko la kimataifa na hoteli za kitalii.

"Niliamua kuja na mradi huu kwa sababu ya changamoto kama nyama inayotakiwa kwenye masoko, mahoteli ya kitalii pamoja na soko la nje ni nyama ambayo iko bora na nyama ambazo zinapatikana ni nyama ambazo hazina kiwango hicho cha ubora" alisema.

Alisema kwa miaka ya karibuni kumekuwa na mahitaji ya nyama ya ng'ombe katika hoteli na masoko ya ndani na nje lakini asilimia kubwa ya nyama nyingi hapa Tanzania zinatokana na ng'ombe wa kienyeji.

"Hatahivyo sasa ng'ombe wa kienyeji wanavyofugwa wakulima wengi wanauza ng'ombe wakiwa na shida ya pesa kwa matumizi ya kulipia karo, kodi au matibabu jambo ambalo huchangia kuuza wanyama dhaifu.

"Tulitengeneza chakula ambacho kinatokana na malighafi ambazo ziko maeneo ya vijijini hasa maeneo ya Kongwa Kijiji cha Mtanana, mwanzo tulifanya utafiti tukaangalia ni vyakula gani ambavyo vipo na vinaweza vikatengeneza chakula cha kunenepeshea ngombe, hivyo tukagundua pumba ya mahindi na mpunga kuongeza na morasesi, mashudu ya alizeti" alisema.

Hata hivyo, alisema wamefanikiwa kutembelea vijiji mbalimbali katika Wilaya ya Kongwa na Meatu mkoani Shinyanga na kubaini kuwa elimu ya unenepeshaji ngombe haipo.

"Hivyo tukaona utafiti wetu utafaa zaidi kwenye Wilaya ya Kongwa Kijiji cha Mtanana A na B, tukajenga banda na kuchukua ng'ombe wenye umri wa miaka miwili au mitatu na kila mfugaji akaleta ng'ombe na kuwapatia aina hizo za chakula kuangalia chakula kipi kitakua bora kwa ajili ya kunenepeshea, kwa siku zipatazo 90 ng'ombe waliongezeka uzito kati ya kilo 50 hadi 100" alisema

Prof. Chenyambuga alisema walifanikiwa pia kuwaunganisha na soko la kisasa Kampuni ya Ranchi ya Taifa NARCO Kongwa na faida mojawapo ni ng'ombe kuuzwa kwa kupimwa uzito, hivyo wafugaji kupata faida kati ya Sh. 160,000 hadi Sh. 235,000 kwa ng'ombe mmoja.

Kadhalika, aliishkuru Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknojia (COSTECH) kwa ufadhili wa Sh. milioni 120 kwa mradi huo kwani wakulima wamefaidika ikiwemo kuwaaunganisha na taasisi za kifedha.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo, Fikiri Robina, alisema amefaidika sana ikiwemo kutoka kwenye kufuga kawaida na kufuga kwa ajili ya biashara.

Meneja wa Ranchi ya NARCO, Elisa Binamungu alisema kuwa Kongwa beef ni nyama pendwa kwa maeneo mengi ya nchi na ina sifa nzuri, hivyo kupelekea kuuza kilo 500 kwa siku.





# Viongozi mitaa wapewa jukumu kuwasaidia watoto wenye uhitaji

**Na Elizabeth John,**
WANGING'OMBE

VIONGOZI wa serikali za mitaa na vijiji mkoani Njombe wametakiwa kuwatambua watoto wenye mahitaji maalumu waliopo katika maeneo yao, kuweka mipango ya kuwasaidia ili wasikatishe ndoto zao za kupata elimu.

Wito huo ulitolewa na Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Wazazi Taifa kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), Belshanza Mhanga wakati akizungumza na waandishi wa habari katoka Kijiji cha Hanjawanu, Kata ya Luduga wilayani Wanging'ombe.

Alisema kutokana na baadhi ya watoto kushindwa kuendelea na masomo yao ipo haja kwa viongozi wa mitaa na vijiji kuwatambua watoto hao na kuweka mipango ya kuwasaidia.

"Wakati umefika sasa kila kiongozi wa kitongoji apate muda wa kwenda katika maeneo yake na wajaribu kutizama familia zenye uhitaji kwa sababu bila ya kufanya hivyo wanaweza wasipate manufaa ya kupata elimu kwa sababu kuna wengine hawajiwezi," alisema Mhanga.

Pia, aliwataka wananchi kukabiliana na vitendo vya ukatili katika maeneo yao, huku akiwataka wazazi kutoa malezi bora na yenye maadili kwa watoto wao.

"Changamoto ninayoiona katika suala zima la malezi waliowengi hawajui wajibu wao kwa hiyo tunatoa wito kwa viongozi wa mitaa hadi vitongoji, madhebu na wadau mbalimbali wapate nafasi ya kuwalea watoto katika maadili mema ili baadaye awe mtu kamili," alisema Mhanga.

Naye Mwinjilisti wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Mtaa wa Hanjawanu, Zera Nwenga alisema bado jamii inawajibu wa kuhakikisha watoto wao wanaendelezwa kielimu kwani huo ndiyo urithi pekee kwa watoto.

"Chakuzungumza na wazazi tujitoe katika kuwasomesha watoto wetu kwa sababu ndiyo watakuja kutusaidia baadaye tutakapokuwa tumechoka, wao watakuwa na nafasi ya kutusaidia sisi wazazi," alisema Nwenga.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Hanjawanu akiwemo, Naomi Ngailo alisema licha ya changamoto zilizopo katika sekta ya elimu bado serikali inatakiwa kutatua changamoto ya miundombinu ya barabara ya kuelekea Ilembula ambayo imekuwa msaada mkubwa kwa shughuli za kiuchumi.

Ngailo alisema: "Changamoto kwenye elimu zipo maana kuna watoto ni watoro lakini pia kwa sababu ya ugumu wa maisha wanaacha shule ila sisi wazazi tutaendelea kusaidiana ili kila mtoto apate elimu itakayomsaidia hapo baadaye".



Viongozi wa CCM wa kata ya Musanja na matawi na baadhi ya wananchi wa kata hiyo, katika jimbo la Musoma Vijijini, mkoani Mara, wakiwa na vitabu vinavyoelezea mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya chama hicho ya mwaka 2020-2025 vilivyotolewa na Mbunge wa jimbo hilo, Prof. Sospeter Muhongo (katikati), mwishoni mwa wiki. PICHA: MPIGAPICHA WETU **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Wazee Kijiji cha Lwangu watakiwa kuripoti matukio ya ukatili

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZEE wa Kijiji cha Lwangu, Kata ya Kifanya, Halmashauri ya Mji Njombe, wametakiwa kutoa taarifa za ukatili pindi zinapotokea ili kuepukana na madhara ikiwemo vifo.

Rai hiyo ilitolewa na mwezeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamiii (TASAF) Kijiji cha Lwangu, Gracian Panza wakati akitoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwa wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya masikini hususani wazee.

"Wazee wamekuwa wakikumbwa na changamoto mbalimbali za ukatili katika jamii haswa wakiwa majumbani na kwenye familia zao, wakati mwengine husababishiwa hata kifo," alisema Panza.

Panza alisema wazee wakinyimwa haki zao ikiwemo kukosa mahitaji muhimu ya binadamu, kunyimwa fursa za maendeleo , kufanyiwa vitendo vya ukatili kama kubakwa na kulawitiwa na wengine kukosa haki ya kuishi kutokana na imani potofu za kishirikina kwa wazee.

"Kuna ukatili mwingine wa kimwili tunatoa adhabu kali mno za kupitiliza iwe ni kwa watoto, unakuta mtoto anapingwa kofi kama mtu mzima hiyo haitakiwi lakini vile vile kina baba tunapiga wake zetu," alisema Panza.

Aidha, aliitaka jamii hiyo kuachana na baadhi ya mila potofu ambazo zinasababisha ukatili wa kijinsia.

"Lakini vile vile kuna ukatili wa kisaikolojia, watu wanatukana sana ukienda kilabuni umekunywa pombe kidogo unatukana wenzio kwa hiyo tabia hizo zote tuziache mara moja, usimtukane mtu," alisema Panza.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kijiji cha Lwangu, Renatusi Masasi aliwaomba wanufaika wa TASAF kuhakikisha wanajiunga na vikundi mbalimbali vya ujasiriamali ili kuweza kujipatia kipato badala yakutegemea fedha

# RC aipa kongole h'shauri kwa kutekeleza maagizo ya Bunge

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, ameupongeza uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa kutekeleza maagizo sita kati ya nane yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) mwaka 2022.

Kanali Abbas alitoa pongezi hizo wakati anazungumza kwenye kikao cha kujadili utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya LAAC kilichofanyika kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea mkoani hapa.

Hata hivyo alizitaja hoja za miaka ya nyuma katika halmashauri hiyo ambazo bado hazijafanyiwa kazi kikamilifu ili ziweze kufungwa ni 12 na kwamba kuna hoja na mapendekezo 53 ambayo yanatakiwa kufungwa na kufanyiwa kazi.

Mkuu wa Mkoa huyo pia aliipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kutekeleza maagizo matano kati ya sita yaliyotolewa na Kamati ya LAAC.

Alisema kati ya maagizo matatu yaliyotolewa na LAAC ni maagizo mawili yametekelezwa na kufungwa, huku agizo moja utekelezaji wake haujakamilika kwa kipindi cha miaka minne sasa.

"Katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea jumla ya hoja na mapendekezo 44 bado hayajafanyiwa kazi ili yafungwe, hivyo nawaomba waheshimiwa madiwani kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha hoja zote zinajibiwa ipasavyo," alisisitiza Kanali Abbas.

Hata hivyo, aliziagiza halmashauri hizo kuhakikisha zinafanya maandalizi ya majibu ya hoja mapema na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wanaozalisha hoja.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Menas Komba, aliahidi kuhakikisha hoja zote zilizosalia katika halmashauri hiyo zinajibiwa na kufungwa sanjari na kusimamia kasi ya ukusanyaji wa mapato.

Naye Mstahiki Meya wa Manispaa ya Songea, Michael Mbano, alisema halmashaur hiyo imejitahidi kutekeleza maagizo sita ya LAAC na kwamba maagizo mawili yaliyosalia itayatekeleza ili yaweze kufungwa.



## Manispaa Mjini Unguja wakusanya bil.4/- makadirio bajeti

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Manispaa Mjini Unguja limesema limefanikiwa kukusanya Sh.bilioni nne (78.7%) ya makadirio ya bajeti.

Mkurugenzi wa baraza hilo, Ali Khamis Mohamed, aliyasema hayo juzi wakati akiwasilisha hotuba ya Makadirio ya mapato na Matumizi ya baraza hilo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Alisema kati ya fedha hizo Sh. bilioni 1.9 ni makusanyo ya ndani sawa na asilimia 57.87 na Sh. bilioni 3.3 ni ruzuku ya mishahara sawa na asilimia 99 ya makadirio.

Khamis alisema baraza hilo linaendelea na jitihada mbalimbali katika kuimarisha mapato ikiwa ni pamoja na kuanzisha maeneo mapya ya uwekezaji.

"Hivi sasa baraza tunatafuta mshauri elekezi kwa ajili ya kuandaa maandiko ya miradi mbali mbali na mipango ya biashara kwa mradi wa Funguni, ujenzi wa eneo la biashara Kwa Alinato, Mikunguni na tunafuatulia na kufanya operesheni za leseni za biashara", alisema.

Aidha, alisema kuwa baraza linasimamia miradi ya maendeleo ya kazi ya ufungaji taa 120 za mitaani katika maeneo ya Kikwajuni, Rahaleo na Chumbuni ambapo hadi sasa taa 60 zimeshafungwa.

Alisema pia baraza linatarajia kujenga jengo la biashara katika eneo la Soko Kongwe la Kwa Hajitumbo ambapo hatua za manunuzi tayari imeshakamilika na wana chosubiri ni mkataba wa ujenzi kutoka serikalini kwa ajili ya kuanza kazi hiyo.

Kuhusu vitambulisho vya wajasiriamali, mkurugenzi huyo alisema katika kuwawekea mazingira bora wafanyabiashara, baraza linaendelea kuwasajili na kuwapatia vitambulisho wafanyabiashara wadogo, kwamba hadi kufikia Machi 22 mwaka huu wafanyabiashara 1,270 wamesajiliwa.

Alisema licha ya utekelezaji huo, baraza linakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo utayari mdogo kwa jamii kushirikiana na manispaa juu ya masuala ya usafi.

"Hivi sasa kuna mlundikano mkubwa wa taka hali inayosababishwa na kukua kwa mji lakini utayari mdogo wa wakazi wa mji katika uhifadhi na udhibiti wa taka", alieleza Khamis.

Wakichangia hotuba hiyo, baadhi ya wajumbe wa baraza hilo, walisema wamefurahishwa na ukusanyaji huo wa mapato, hivyo kulitaka baraza kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa kutafuta wawekezaji katika maeneo mbali mbali.Naye Diwani wa Amani, Makame Khamis Ame, alisema ipo haja kwa baraza kuongeza programu za uhamasishaji jamii juu ya masuala ya usafi kupitia luninga, redio, mikutano ya jamii na shule ili kuimarisha usafi kwa maeneo mbalimbali ya mji.

Diwani wa Mlandege, Kinunu Rashid Slim, alisema ni vyema kwa baraza kutia nguvu katika matumizi ya kanuni ya papo kwa papo ili kuweka nidhamu katika mji na kuongeza vyanzo vipya vya mapato.

# 'Hakuna sheria inayozuia watu kula mchana wakati wa mfungo'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar limetoa ufafanuzi kuhusu operesheni kamatakamata ya wananchi wanaokula hadharani wakati wa mwezi wa Ramadhani visiwani hapa, likisema hakuna sheria ya kuwazuia watu kula wakati wa mfungo.

Kamishna wa Jeshi hilo visiwani hapa, Hamad Khamis Hamad alitoa ufafanuzi huo wakati wa mahojiano maalumu na gazeti hili ofisini kwake.

Nipashe lililazimika kupiga hodi ofisini kwa kamishna huyo ili kufahamu tuhuma zilizopo dhidi ya Jeshi la Polisi visiwani Zanzibar kuwakamata watu waokula mchana katika kipindi hiki cha Ramadhani.

Kamishna huyo alisema jeshi hilo halina mamlaka hayo kwa sababu Zanzibar hakuna sheria ya karipio la watu kuwazuwia kula mchana katika mwezi wa Ramadhani.

"Hakuna sheria inayokataza watu wasile mchana wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhani. Ukiondoa imani ya dini ya Kiislamu na jeshi hilo husimamia operesheni zinazofanywa na mamlaka zingine za serikali ili zifanyike kwa amani na usalama" alisema.

Aidha, alisema kumekua na mkanganyiko wa taarifa kuhusu jeshi hilo kukamata watu ambao walikuwa wakivuta bangi mchana katika mwezi huu wa Ramadhani na siyo operesheni ya watu kula mchana kwa sababu bangi ni kosa la jinai.

"Nilitoa maelekezo ya kwamba kufanyike operesheni kwa wale wanaovuta bangi kwa sababu ni kosa la jinai, lakini shida iliyojitokeza kwamba operesheni hiyo ilikamata waliokuwemo na wasiokuwemo ambapo ilikamata waliovuta bangi na waliokuwa wakila mchana mwezi huu wa Ramadhani wakati kula mchana siyo kosa kisheria" alisema.

Alisema Jeshi la Polisi halina mamlaka ya kuwakamata watu wanaokula mchana mwezi wa Ramadhani isipokuwa kuna mamlaka zingine za serikali kwa kutumia sheria wanaweza wakafanya operesheni hizo.

Alisema jukumu la Jeshi la Polisi ni kusimamia operesheni hizo ili kufanyika kwa amani na utulivu.

Mwanasheria wa kujitegemea visiwani Zanzibar, Hassan Kijogoo, alisema Zanzibar hakuna sheria inayokataza watu kula mchana mwezi wa Ramadhani na watu wanachanganya sheria za dini na za nchi.

Alisema watu wanaoguswa na hilo wanaweza kushawishi kupeleka mswada kupendekeza kuwa sheria ya watu kutokula mchana wakati wa mwezi wa Ramadhani.

Kijogoo alisema: "Kula mchana mwezi wa Ramadhani siyo jinai, polisi wanahusika na makosa ya jinai ya yapo mengi kama kuiba, kubaka, kuuza na kula dawa za kulevya lakini kula mchana mwezi wa Ramadhani siyo kosa la jinai na polisi sio jukumu lao kuwasaka watu wanaokula mchana na kufanya hivyo wanafanya makosa".



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Mudrik Ramadhani Soraga akitoa wasifu wa Marehemu Kanali mstaafu Said Iddi Bavuai ambaye ni miongoni mwa waasisi wa mapinduzi ya Zanzibar, baada ya kusoma dua katika kaburi lake huko Shakani, Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya kuwaenzi viongozi wa Kitaifa na waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: MAELEZO - ZNZ**

# Polisi yakishukia ACT-Wazalendo usambazaji taarifa potofu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, amekitaka Chama cha ACT-Wazalendo kuacha kutumia mitandao ya kijamii kusambaza taarifa za kupotosha kuhusu hali ya uhalifu na usalama kwa malengo yao binafsi ya kisiasa.

Alitoa tahadhari hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika makao makuu ya jeshi hilo visiwani hapa, kufuatia taarifa iliyotolewa na chama hicho iliyoasainiwa na Katibu wa Habari, Uenezi, Mawasiliano na Umma, Salim Bimani.

Kamishna Hamad alisema kinyume na madai ya upotoshaji yanayotolewa na chama hicho ya uwepo wa vikundi vya kihalifu vinavyojiimarisha kila siku pasipo Jeshi la Polisi kuonesha uwezo wa kudhibiti kwa kukinga au kufanya upelelezi unaosababisha wahusika kutiwa hatiyani.

"Napenda niwahakikishie wananchi kuwa madai haya lengo lake ni kuzusha hofu na taharuki. Ni uthibitisho wa utamaduni endelevu wa baadhi ya viongozi wa chama hicho kutothamini juhudi za serikali na taasisi zake katika kudumisha amani na utulivu" alisema kamishna huyo.

Alisema viongozi wa ACT-Wazalendo wanapaswa kutambua uhalifu ni zao la jamii na udhibiti wa uhalifu ni jukumu la jamii na wao kama sehemu ya jamii wanawajibu wa kushirikiana na serikali pamoja na vyombo vinavyotekeleza sheria katika kubaini visababishi vikundi vya uhalifu kama ukosefu wa malezi, umasikini na ukosefu wa maadili.

Alisema pia wanapaswa kushiriki katika kutengeneza sera na mikakati madhubuti ya kijamii na kiuchumi badala ya kujiweka pembeni kubuni mikakati ya kuwajengea hofu wananchi.

"Sote tunatambua nguvu ya vyama vya siasa katika kuwezesha ubia na ushirikiano kati ya vyombo vinavyotekeleza sheria na jamii, katika kuunga mkono progaramu mbalimbali za kubaini na kuzuia uhalifu kama vile polisi jamii, ambayo lengo lake ni kuwashirikisha wananchi katika kutambua viashiria vya uhalifu na kuvishughulikia kabla ya uhalifu haujatokea.

Aidha alisema wanasiasa kupitia majukwaa yao ya kisiasa wanaweza kuongeza ufahamu kwa umma juu ya umuhimu wa kuunga mkono juhudi za vyombo vinavyotekeleza sheria za kubaini na kuzuwia uhalifu na kudumisha usalama wao.

"Ni kwa bahati mbaya baadhi ya viongozi wa ACT-Wazalendo hapa Zanzibar wakiwashawishi wananchi wasijiunge na vikundi vya ulinzi shiriki kwa madai kuwa ulinzi shirikishi ni sera ya chama kilicho madarakani" alisema Kamishna Hamad.

Alisema usalama wa raia na mali, hali ya amani na utulivu katika nchi hunufaisha watu wote bila kujali tofauti za itikadi, uwezo au hali ya mtu.

Hata hivyo alisema athari kubwa za usambazaji taarifa potofu na za kutia chumvi kwenye jamii na kwa kutumia mitandao ya kijamii zinaweza kuzusha hofu na wasiwasi hata kama hatari halisi ya kutendewa uhalifu ni ndogo, kuchochea ubaguzi na mgawanyiko, kudhoofisha juhudi za kukuza ushirikishwaji wa jamii yakijumuisha ulinzi na usalama.

Kamishna Hamad aliwaasa viongozi wa chama hicho hasa wale wanaotumia nafasi zao kusambaza taarifa za upotoshaji zinazoweza kuleta hofu na taharuki kwa jamii kuacha tabia hiyo.

# HABARI PICHA




Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (kulia), akisalimiana na viongozi wa chama hicho baada ya kuwasili jijini Dar es Salaam jana, kuanza ziara ya siku moja ambapo alitarajiwa kujumuika na viongozi na wawakilishi wa makundi mbalimbali ya kijamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Magari yakipita kwenye dimbwi kubwa la maji ya mvua yaliyotuama katika eneo la Kiziani Kitunda, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mzee wa Kanisa la Waadventista Wasabato Muheza Central, wilayani Muheza mkoani Tanga, John Mdoe (kulia), akiwakaribisha viongozi wa dini, wakati wa futari aliyoiandaa nyumbani kwake mtaa wa Mdote juzi. Wapili (kulia) ni Mchungaji wa kanisa la Sabato Michungwani Muheza mjini, Daud Masindi, (watatu kulia) Shekhe wa wilaya hiyo, Abdallah Seif, Katibu wa BAKWATA wilaya, Shabani Nguzo na (kushoto) ni Mchungaji wa kanisa la Sabato Kana jijini Tanga, Mbonea Mshota. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Maendeleo la Bonde (BDF) ambaye pia ni Diwani wa Viti Maalum Tarafa ya Ngomeni, wilayani Muheza mkoani Tanga, Fatuma Kweka (katikati), akikabidhi kiti mwendo kwa Ofisa Maendeleo ya jamii wa wilaya hiyo, Stella Kategile hivi karibuni, kilichotolewa msaada na jukwaa hilo, kwa ajili ya watoto wenye uhitaji maalum. Wengine ni Mjumbe wa jukwaa hilo, Lameck Kishiwa (kushoto), Katibu wa jukwaa hilo, Zacharia Mhina (wa pili kushoto) na Ofisa Elimu maalum wa wilaya hiyo, Sudi Wabu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Muuza supu akifanya shughuli zake katika barabara ya Sewa, Mikocheni kiwandani, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wake. **PICHA: BEATRICE MOSES**

## Rais Tshisekedi amteua Judith Waziri Mkuu DRC

**KINSHASA,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi amemteua Waziri wa Mipango, Judith Suminwa kuwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo.

Judith ni mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo wa Waziri Mkuu nchini Congo. Ikielezwa kuwa uteuzi wake unakamilisha wiki kadhaa zilizoghubikwa na hali ya sintofahamu kuhusu wadhifa huo.

Katika hotuba aliyoitoa jana kupitia televisheni ya taifa, Judith alisema kuwa anafahamu kuhusu jukumu kubwa linalomkabili na kuongeza kuwa atafanya kazi kuhakikisha kuweko kwa amani na maendeleo nchini humo.

Kuapishwa kwa Tshisekedi kwa muhula wa pili madarakani mnamo mwezi Januari, kulianzisha mchakato wa muda mrefu wa kutafuta muungano wa vyama vingi katika bunge la kitaifa, hatua muhimu kabla ya kuteuliwa kwa waziri mkuu na kuundwa kwa serikali.

Serikali ya nchi hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi zinazojumuisha mgogoro unaozidi kutanuka na mzozo wa kibinadamu katika maeneo ya Mashariki mwa nchi hiyo pamoja na usimamizi wa madini. **DW**



# Wanajeshi wanaolinda amani DRC walalamikia kukosa silaha

**KINSHASA,** DRC

WANAJESHI wa Afrika Kusini waliopelekwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kusaidia kuleta utulivu wamesema baadhi yao hawana silaha na wanatarajiwa kupambana na waasi wa M23 bila msaada wa helikopta za usafiri.

Mwezi Februari mwaka huu, Serikali ya Afrika Kusini ilipeleka wanajeshi 3,000 kujiunga na wengine 1,000 ambao tayari walikuwa katika eneo la mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambayo imekumbwa na vita ambavyo vinasababishwa na magenge yenye silaha.

Wakati huo, Pretoria ilisema kupelekwa kwa wanajeshi hao ilikuwa sehemu ya dhamira yake ya kulinda amani barani Afrika, na kuisadia DRC kukabiliana na mashambulizi ya waasi.

Licha ya adhima hiyo nzuri kwa sasa, wanajeshi hao wanasema hawana vifaa vya msingi, jambo linaloweza kuwaweka katika hatari kubwa.

Aidha, ilibainishwa kuwa Afrika Kusini inakabiliwa na changamoto kadhaa za kiuchumi.

**Kando na hayo, kuna changamoto za kifedha mbali na uwezo wa wanajeshi hawa. Hakuna ndege ya kubeba vifaa muhimu ambavyo wanajeshi wanahitaji walipopelekwa ili kuwasaidia kikamilifu.**

Waziri wa Ulinzi, Thandi Modose, aliwaambia waandishi wa habari hivi karibuni mjini Pretoria kwamba helikopta tano tu za usafiri kati ya 39 ndizo zinafanya kazi, na kwamba ni helikopta tatu tu kati ya 11 za kufanya mashambulizi ndizo zinaweza kuruka.

Wizara yake inakiri kuwa ilishindwa kusaini kandarasi mpya na kampuni ya kutunza na kukarabati ndege hizo.

Wanajeshi nchini DRC walisema pia kwamba hawapati huduma za madaktari na wauguzi, na wakati mwingine hulala njaa baada ya kukosa chakula.

Kiongozi wa chama cha jeshi la taifa Pikkie Greeff, alisema serikali ilipeleka wanajeshi wake katika moja ya maeneo hatari zaidi ya vita duniani bila vifaa, ufadhili na mafunzo muhimu.

"Wanajeshi wa Afrika Kusini wanalazimika kuweka kambi mpya, wakiwa pia na fikra ya kushambulia sio kujilinda. Hiyo ni njia mpya ya kujifunza kwa jeshi kwa sababu hatujafanya mazoezi hayo. Usipofanya mazoezi mara kwa mara, hautatekeleza vizuri.

"Kando na hayo, kuna changamoto za kifedha mbali na uwezo wa wanajeshi hawa. Hakuna ndege ya kubeba vifaa muhimu ambavyo wanajeshi wanahitaji walipopelekwa ili kuwasaidia kikamilifu," alisema

Hata hivyo, ilielezwa kuwa tangu mwezi Februari, waasi wa M23 wameua wanajeshi kadhaa wa Afrika Kusini wanaopigania ardhini, na kujeruhi wengine kadhaa katika shambulio la kombora.

Greeff alisema anazungumza na wanajeshi walioko DRC kila siku, na ari yao iko chini. Na kwamba wengine wanahisi kwamba wako katika operesheni ya kujiua.

"Watu hawa wako katika hatari kubwa. Kupelekwa kwao kuliamualiwa kwa haraka sana. Kama kulikuwa na mpango, mpango huo haukujadiliwa kwa uwazi kwa sababu kwa hakika wanajeshi walio uwanjani wanaachwa katika hali ngumu kwa sababu ya uhaba huu wa vifaa na mambo mengine. Hali ni tete sana," alisema.

Akizungumza bungeni hivi karibuni, Rais Cyril Ramaphosa alikanusha kuwa utawala wake ulipeleka wanajeshi nchini DRC kwa maslahi na bila msaada unaohitajika.

Vile vile, alisisitiza kuwa wanajeshi wake wako tayari kupigana na wana uwezo wa kutosha.

Licha ya kauli hiyo Greeff alisema wanajeshi zaidi wa Afrika Kusini watajeruhiwa na kuuawa nchini DRC, iwapo hawatapata uwezo.

Wachambuzi wa masuala ya kijeshi na ulinzi wanasema nia ya serikali ya Afrika Kusini ya kulinda amani hailingani na fedha zinazohitajika ili kuhakikisha mafanikio yao. **VOA**



Wananchi wakisukuma gari baada ya shambulio la Israel lililotekelezwa kulenga jengo lililo jirani na ubalozi wa Iran mjini Damascus, Syria ambalo Iran imethibitisha limeua maofisa wake kadhaa wa jeshi akiwamo kamanda wa juu kwenye jeshi lake, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Israel, Marekani kujadili vita mji wa Rafah, Gaza

**JERUSALEM,** Israel

MATAIFA ya Israel na Marekani yanafanya mazungumzo kuhusu mpango wa uvamizi wa ardhini wa vikosi vya Israel kwenye mji wa Rafah huko katika Ukanda wa Gaza.

Inaelezwa kuwa mazungumzo hayo yatafanyika kwa njia ya mtandao wiki moja baada ya Israel kuifutilia mbali safari iliyokuwa imepangwa ya kutuma ujumbe wake mjini Washington.

Mivutano kati ya washirika hao wawili imeongezeka kutokana na idadi kubwa ya vifo vya raia vinavyoshuhudiwa Ukanda wa Gaza yanayoibua shaka kubwa zaidi mjini Washington juu ya dhamira ya Israel ya kutaka kufanya operesheni ya kijeshi kwenye mji uliofurika watu wa kusini mwa Gaza wa Rafah.

Israel ilifuta ziara yake ya mjini Washington baada ya Marekani kutotumia kura yake ya turufu kuzuia azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linalotoa mwito wa kusitishwa vita vya Gaza. Na kwamba Marekani ilijizuia kulipigia kura azimio hilo.

Katika hatua nyingine wakosoaji wa sera za Serikali ya Israel wamepiga kambi kwenye mahema mbele ya majengo ya bunge mjini Jerusalem, ikiwa ni sehemu ya maandamano yaliyoingia siku ya nne.

Waandamanaji hao wanashinikiza serikali ijiuzulu, kuitishwa kwa uchaguzi mpya na kuachiliwa kwa mateka wanaoshikiliwa na kundi la Hamas. **DW**

# CRDB YADHAMINI FA CUP KWA BILIONI 3.7/-

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limeingia ushirikiano na Benki ya CRBD wa mkataba wa miaka mitatu na nusu wa kuwa Mdhamini Mkuu wa Kombe la Shirikisho la Soka nchini maarufu FA Cup wenye thamani ya Sh. bilioni 3.79 pamoja na VAT.

**Utiaji saini huo umefanyika katika makao makuu ya Bank hiyo jana, huku udhamini huo ukianzia hatua hii ya 16-bora ya Kombe la FA baada ya makubaliano hayo kufikiwa kati ya TFF na CRBD Bank.**

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRBD, Abdulmajid Nsekela, alisema hivi karibuni walikuwa na ushirikiano na klabu za soka hapa nchini na sasa wameona wauendeleze zaidi kwa kushirikiana na TFF katika kuendeleza soka la Tanzania.

Alisema wameingia makubaliano hayo kwa hatua ya 16-bora ambapo kwa kuanzia hapo wametoa kiasi cha Sh. milioni 255 kwa ajili ya kumalia hatua hiyo na baadae wataendelea kwa misimu mingine.

"Udhamini huu unaenda kuboresha mambo mbalimbali ila kwa sasa tumeamua kutoa kiasi cha Sh. milioni 255 kumalizia hatua hii ya 16-bora ambayo inaanza kuchezwa leo (jana) kati ya Namungo FC na Kagera Sugar.

"Tumeona jinsi ambavyo TFF inavyosimamia soka na kufanya vizuri kwa timu za taifa ikiwamo Taifa Stars, Twiga Stars na timu za vijana kuipeperusha vema bendera yetu ya Tanzania," alisema Msekela.

Kwa upande wa rais wa TFF, Wallace Karia, alisema ni tukio la kihistoria kwa kusaini mkataba wa udhamini mkuu wa kwanza katika mashindano haya ya Kombe la Shirikisho ambayo awali ilijulika kama Azam Sport Federation na sasa inaenda kuwa CRDB Bank Federation.

Alisema mchakato umehitimishwa jana baada ya mazungumzo ya muda mrefu na CRDB kuwa wadhamini wa kwanza wa mashindano hayo ambaYo awali yalikuwa chini ya Azam kwa sababu ya kuwa na haki za kuonyesha michezo hiyo.

"Kwa mara ya kwanza Kombe la Shirikisho linapata mdhamini mkuu ambaye ni CRBD Bank kwa mkataba wenye thamani ya Sh. bilioni 3.2 baada ya VAT, mashindano haya yanashirikisha timu nyingi zaidi ya 100, yanaamzia chini tangu level ya wilaya.

"Ninaimani mashindano ya CRBD Bank Federation yanaenda vizuri na fedha zitaenda katika sehemu husika kwa timu kusaidia mambo mbalimbali ikiwamo usafiri na mahitaji muhimu," alisema Karia.

Aliongeza kuwa wao kama shirikisho walikutana na kuona fainali za FA, msimu huu zitafanyika katika Uwanja wa Tanzanite uliopo Babati mkoani Manyara, baada ya kujiridhisha na ubora wa miundombinu yao ikiwamo uwanja.

Aidha, alisema msimu huu nusu fainali zitakuwa mbili, moja itafanyika jijini Mwanza na ya pili bado haijulikana mkoa gani itacheza kwa sababu ya mikoa kuendelea kufanya ukarabati wa viwanja vyao.

## Wachezaji Coastal Union waingizwa darasani

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA hali ambayo haikuzoeleka, Kocha Mkuu wa Coastal Union, David Ouma, ameanza mazoezi na kikosi chake kwa kuwaingia darasani badala ya uwanjani kama ilivyozoeleka.

Kocha huyo akiwa na kikosi chake na watu wake wa benchi la ufundi wameanza mazoezi ya darasani kwa ajili ya kuwafundisha vitu mbalimbali vya soka kinadharia ili wachezaji wapate kumsikiliza kwa makini wakiwa wametulia.

Klabu ya Coastal Union, imechapisha picha kwenye moja ya akaunti yake ya mtandao wa kijamii, ikionyesha kocha huyo akiwa bize amesimama mbele ya wachezaji akiwaeleza mambo mbalimbali wanayotakiwa kufanya wakiwa uwanjani, huku wachezaji wake wakiwa wamekaa kwenye viti na madawati kama wanafunzi, wakiwa na jezi za klabu hiyo na wakisikiliza kwa makini.

Kocha huyo amesema jana kuwa, mwalimu siku zote anatakiwa kufundisha kwa vitendo na kwa maneno pia, hivyo amewaingiza darasani kipindi hiki ambacho wametoka kwenye mapumziko, kabla ya kuingia gym, na hatimaye uwanjani.

"Siku zote mwalimu kazi yake ni kufundisha kwa mbinu zote, ili mradi ni kuhakikisha malengo yanatimia," alisema Ouma.

Ofisa Habari wa Coastal Union, Abbas El Sabri, amesema hiyo yote ni mipango ya viongozi na mwalimu, ambapo uongozi umempa kocha kila anachohitaji kuhakikisha malengo ya kumaliza ligi wakiwa nafasi ya nne na kucheza mechi za kimataifa msimu ujao yanafanikiwa.

"Hii ni mipango ya kuhakikisha kwanza tunaingia robo fainali ya Kombe la FA, na Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema El Sabri.

**TUPO PAMOJA...**



Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Lukiza Autism Foundation, Hilda Nkabe, akicheza ngoma na mtoto mwenye usonji katika Shule ya Msimbazi Mseto jijini Dar as Salaam jana, ikiwa ni Siku ya Usonji duniani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Zimamoto wapania ubingwa FA Cup

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Zimamoto SC imesema sasa inaelekeza nguvu na mipango yake mikubwa katika kuhakikisha inatwaa ubingwa wa michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup.

Zimamoto SC katika hatua ya 16-bora itakutana na na Wafalme wa Kinyasini, New King FC, timu ambayo ipo daraja la kwanza Kanda na imekuwa ikifanya vizuri katika michuano hiyo kwa kufika hatua ya nusu fainali kwa misimu mitatu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Zimamoto Mohmed Hilali 'Tedi', alisema timu hiyo haikuvunja mazoezi kama ilivyozoeleka katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani ili kujiandaa na michuano hiyo.

Alisema lengo kuu la kuendelea na mazoezi katika mwezi huu wa Ramadhani ni kuhakikisha inatimiza malengo yao waliyojiwekea ya kulitwaa Taji la FA au Ligi Kuu Zanzibar.

Tedi alisema baada ya timu hiyo kukosa nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa takriban misimu minne sasa, msimu huu mpango wao ni kuhakikisha wanapata ushiriki kati ya mataji hayo mawili huku ubingwa wa FA wakiutilia mkazo zaidi.

"Tunataka kuhakikisha tunafanya vizuri katika michuano hii ya Kombe la FA, tunajua 'tosi' yetu imedondokea kwa timu ngumu New King FC, hivyo lazima tujipange kwakuwa mchezo wa soka upo katika bahati, lakini pia jitihada za kiuchezaji," alisema.

Aidha, alisema licha ya maandalizi makubwa wanayofanya kwa ajili ya Kombe la FA. lakini bado wanaendelea na mipango yao kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar ambao unaushindani mkubwa.

"Tunachanga karatasi zetu kwa ajili ya FA, lakini bado tutaendelea kuzichanga kwa ajili ya ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, tunajua ushindani bado ni mkubwa na ukaribu wa alama kwa aliyepo kileleni mpaka nafasi ya nne ni mdogo sana, hivyo tunataka kuhakikisha vyote tunafanya vizuri ili kutimiza lengo letu," alisema.

Michuano hiyo ya FA Cup katika hatua ya 16 bora itaendelea mapema Aprili 18, mwaka huu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### AWINDWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inatarajiwa kurejesha azma yao ya kumnunua mlinda lango wa Arsenal, Aaron Ramsdale, 25, msimu huu wa majira ya joto huku wakimlenga kipa mwenye umri mdogo zaidi. ***(Mail)***

### MESSINHO KUPOTEZEWA

BARCELONA imesitisha mpango wa kumnunua Estevao Willian, 17, kutoka Palmeiras ya Brazil ambaye amepewa jina la 'Messinho', katika hatua inayotoa nafasi kwa Chelsea na Paris St-Germain kumsajili. ***(Sport)***

### GIBBS-WHITE MILIONI 50

TOTTENHAM Hotspur na Newcastle United zimeambiwa zitalazimika kulipa zaidi ya pauni milioni 50 iwapo zinataka kumsajili kiungo wa England, Morgan Gibbs-White, 24, kutoka Nottingham Forest, ambaye huenda ikalazimika kumuuza kwa sababu ya matatizo yao ya kifedha. ***(Football Insider)***

### ALONZO KUONDOKA BARCA

MLINZI wa Barcelona na Hispania, Marcos Alonso, 33, anatarajiwa kuondoka bila malipo msimu huu wa majira ya joto, huku kiungo wa kati wa Hispania, Sergi Roberto pia akiondoka bila malipo. ***(Fabrizio Romano)***

### ONANA KUWEKWA SOKONI

KLABU ya West Ham italazimika kulipa pauni milioni 60 kama inataka kumsajili kiungo wa kati wa Everton na Ubelgiji, Amadou Onana, 22. ***(Football Insider)***

### PHILLIPS KUFUNGWA CITY

KLABU ya Manchester City inatarajiwa kumsajili kwa mkataba wa kudumu kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips, 28. ***(Mail)***

### ADARABIOYO AGOMBEWA

LIVERPOOL, Tottenham Hotspur na AC Milan ziko tayari kupigania saini ya beki wa Fulham, Tosin Adarabioyo mwenye umri wa miaka 26, kwa uhamisho wa bure msimu huu wa majira ya joto. ***(Sun)***

### JAMES ATAKIWA MADRID

KLABU ya Real Madrid inatathmini uwezekano wa kumsajili beki wa kulia wa Chelsea na England, Reece James, lakini wanatarajia dili lolote kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, kuwa gumu kwa sababu amesalia na miaka minne kumaliza mkataba wake. ***(Fichajes)***


### ISAK ASAKWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inajiandaa kupokea ofa kutoka kwa Arsenal na Tottenham Hotspur, ambazo huenda zikagharimu pauni milioni 100, kwa mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak, 24. ***(Sun)***

### PHILLIPS AWANIWA LEEDS

LEEDS United inapania kumsajili tena kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 28, kwa takribani pauni milioni 30 kutoka Manchester City msimu huu wa majira ya joto. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR ADOKEZA TENA KUONDOKA SAUDI ARABIA

**SAO PAULO,** Brazil

## Amewaambia wachezaji wa Santos, aliporejea Brazil kuitazama timu yake...

NEYMAR anatazamia kuondoka Saudi Arabia na amewaambia wachezaji wa klabu yake ya zamani ya Santos kwamba atarejea Brazil ifikapo 2025, kwa mujibu wa ESPN.

**Winga huyo mwenye umri wa miaka 32, aliondoka Paris Saint-Germain na kujiunga na Al Hilal msimu wa majira ya joto kwa dau la euro milioni 90, lakini akaumia kwenye mechi tano tu katika maisha yake ya soka nchini Saudi Arabia.**

Mkataba wake unaaminika kuwa na thamani ya karibu euro milioni 150 kwa msimu.

Huku akiwa hayupo, Neymar alirejea Brazil kuitazama timu ya zamani ya Santos ikimenyana na Palmeiras katika fainali ya Campeonato Paulista, na kwa mujibu wa UOL Esporte, ndipo alipotangaza kwa faragha mpango wake wa kuondoka Saudi Arabia.

Neymar anaripotiwa kuwaambia wachezaji na wafanyakazi wa Santos kwamba anapanga kucheza katika msimu wa 2025 wa Brazil, ambao unatarajiwa kuanza Aprili 2025 - miezi miwili kabla ya mkataba wake na Al Hilal kumalizika.

Winga huyo aliwahi kuzungumzia nia ya kurejea Brazil wakati fulani sasa ni dalili kwamba Neymar ana mpango wa kuondoka Saudia.

Neymar alionesha kiwango kizuri katika wiki za mwanzo za muda wake nchini Saudi Arabia, akitengeneza pasi tatu za mabao na kufunga katika mechi tano kabla ya kuumia.

Licha ya kukosekana kwake, Al Hilal wamebakia kileleni mwa msimamo wakiongoza kwa pointi 12, wakiongozwa na mshambuliaji wa zamani wa Fulham, Aleksandar Mitrovic aliyefunga mabao 22.

Sergej Milinkovic-Savic na Ruben Neves wanaongoza katika chati za wasaidizi wa klabu hiyo, huku winga wa zamani wa Barcelona, Malcom pia akiwa amefunga mabao 14 na kutoa pasi za mabao kumi katika michuano yote.

Al Hilal wanatarajiwa kuwika msimu huu wa majira ya joto na wanatarajiwa kushinikiza kumsajili fowadi wa Liverpool, Mohamed Salah, ambaye analengwa zaidi na Saudi Pro League pamoja na kiungo wa Manchester City, Kevin De Bruyne.

HABARI MICHEZO



# AMORIM APUUZIA KWENDA LIVERPOOL

**LISBON,** Ureno

KOCHA wa Sporting CP, Ruben Amorim, amepuuzilia mbali uvumi kuhusu hatma yake na kusema kwamba kushinda mataji msimu huu katika klabu hiyo ya Ureno ndicho kipaumbele chake kikuu.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 39, amekuwa akihusishwa na kuchukua jukumu la kuinoa Liverpool, huku Jurgen Klopp akitarajiwa kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

Uvumi kuhusu mustakabali wa Amorim umeshika kasi katika siku za hivi karibuni huku bosi wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso - akisema mustakabali wake ni kubakia kwenye klabu hiyo ya Bundesliga.

"Kocha wa Sporting ndio pekee wa Sporting," alisisitiza Amorim.

"Wachezaji wanajua ni kiasi gani wanataka kushinda na ninataka kushinda mataji kwa Sporting. Wako wazi kwamba kila mtu analenga kushinda mataji."

Amorim alikejeli ripoti kwamba Sporting tayari wamepanga mrithi wake, Anthony Barry mwenye umri wa miaka 37, ambaye ni Kocha Msaidizi wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ureno.

"Kitu pekee kinachoniudhi ni kwamba tayari walikuwa na mbadala wangu," alitania Amorim.

"Hilo ndilo lililonikera zaidi, hata nilimwambia Viana Hugo Viana, Mkurugenzi wa Soka wa Sporting atulie kwa sababu si hivyo."

Mtindo wa uchezaji wa kushambulia wa Amorim umevutia watu wengi katika miaka yake minne ya kuinoa Sporting na tayari ameshinda taji la Ligi ya Ureno na mataji mawili ya ligi katika klabu hiyo.

# *Varane alia na maumivu ya kichwa*

**MANCHESTER,** England

MLINZI wa Manchester United, Raphael Varane, amesema kuumia mara kwa mara katika maisha yake ya soka, kumeharibu mwili wake.

Varane mwenye umri wa miaka 30, aliliambia Jarida la Ufaransa L'Equipe kwamba amecheza michezo mingi kwa klabu na nchi huku akikabiliana na madhara ya majeraha ya kichwa.

Mchezaji huyo wa zamani wa Kimataifa wa Ufaransa, ambaye alistaafu soka ya kimataifa Februari 2023, alisema alichanganyikiwa wakati akiichezea nchi yake kwenye hatua ya 16-bora ya Kombe la Dunia 2014 dhidi ya Nigeria, na kuongeza kwamba alimaliza mchezo akiwa hajielewi na kwamba "ikiwa kuna mtu alizungumza nami wakati huo, sijui kama ningeweza kujibu."

Varane alisema pia alicheza akiwa na dalili za jeraha la kichwa akiwa na Real Madrid dhidi ya Manchester City kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2019-20 ulioathiriwa na COVID-19.

Suala hilo linaendelea kumuathiri Varane na kumfanya akose mechi msimu huu kwa Man United - haswa kuhusiana na "mishtuko midogo" inayosababishwa na mipira ya kichwa.

"Mara ya kwanza niliposikia kuhusu kuchanganyikiwa ilikuwa msimu huu ambapo wataalamu walikuja kuzungumza nasi kuhusu hilo... mara nyingi, kama mchezaji, hatuelewi na hata hatufikirii kufanya mtihani," alisema.

"Mapema msimu huu, nilipiga mpira kwa kichwa mara kwa mara wakati wa mechi ya Man United na nilihisi uchovu usio wa kawaida katika siku zilizofuata, na pia kuwa na uchovu wa macho.

"Niliripoti kwa wafanyakazi ambao walipendekeza sana nisicheze, na nilifanya mtihani ambao ulimaanisha kwamba nitakosa mechi iliyofuata."



# Ancelotti: Real wana faida zaidi ya Manchester City

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amekiri kuwa timu yake itakuwa na faida zaidi ya Manchester City katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kutokana na ratiba yao kuwa nyepesi.

'Los Blancos' hao watacheza na Man City katika hatua ya robo fainali, na mechi ya kwanza itafanyika Santiago Bernabeu Jumanne ya April 9, kabla ya mechi ya marudiano kwenye Uwanja wa Etihad Jumatano ya Aprili 17, mwaka huu.

Hata hivyo, kocha wa City, Pep Guardiola alifichua kuchoshwa kwake na mpangilio wa mechi wiki iliyopita huku timu yake ikiwa na ratiba ya Ligi Kuu England, wakati Madrid watakuwa na siku tisa za mapumziko.

"Tunacheza na Aston Villa saa 2:15, kisha saa 6:30 dhidi ya Crystal Palace Jumamosi," alisema Guardiola.

"Kisha tunaenda Madrid Jumanne. Madrid ina siku tisa za kujiandaa.

"Wanacheza wikendi hii na hawatacheza tena hadi mchezo wetu. Ningependa kutafakari na kuomba siku moja zaidi, kwa sababu tofauti ni kubwa."

Kutokana na ushindi wa mabao 2-0 wa Madrid nyumbani dhidi ya Athletic Club Jumapili jioni, Ancelotti aliulizwa maoni yake juu ya maoni ya Guardiola na akakubali kwamba timu yake itakuwa na faida.

"Naiona vizuri, wana ratiba ngumu zaidi, ni soka la kisasa," alisema Ancelotti.

"Ni dhahiri kwamba tuna faida ndogo, lakini haitaathiri mechi."



Madrid wamepangwa na City katika hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa kwa msimu wa tatu mfululizo baada ya kukutana nao katika nusu fainali katika kila moja ya kampeni mbili zilizopita.

Mshindi wa mechi hii atakutana na Arsenal au Bayern Munich katika nusu fainali, huku Atletico Madrid, Borussia Dortmund, Paris Saint-Germain na Barcelona zikicheza upande mwingine wa droo.

## Pacome ampa mzuka Gamondi

INATOKA UKURASA 24

Aliongeza kuwa Mamelodi Sundowns ni wazuri, lakini amejipanga kukabiliana nao katika mchezo huo wa ugenini kuhakikisha wanafanikiwa kupata ushindi ugenini jambo ambalo kwenye mpira linawezekana.

Gamondi alisema kazi kubwa anayoifanya kwa siku chache ni kuwajenga kisaikolojia wachezaji wake kutocheza kwa presha hasa safu ya ulinzi na ushambuliaji kuwa makini.

Katika hatua nyingine, Yanga ilieleza kupata mapokezi mazuri kutoka kwa Balozi wa Tanzania nchini Misri, James Bwana, baada ya kuwasili jana mchana.

Jana Serikali kupitia Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma maarufu Mwana FA, alisema imezitaka balozi zake nchini Afrika Kusini na Misri kuhakikisha zinahakikisha usalama unapatikana kwa Yanga na Simba zikiwa Afrika Kusini na Misri.

Simba nayo imeondoka leo alfajiri kuelekea Misri tayari kwa mchezo wao wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ambao nao utachezwa Ijumaa wiki hii.

## Lina kuenziwa kwa Gofu Moro

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya Gofu yaliyofanyika Moshi, Kilimanjaro hivi karibuni ya kumuenzi mchezaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya Wanawake ya Gofu, Lina Nkiya, kwa sasa yanatarajiwa kufanyika mkoani Morogoro Aprili 11, mwaka huu, imeelezwa.

Michuano hiyo inayoitwa Lina PG Tour, imeandaliwa na familia ya Said Nkya kwa kushirikiana na Chama cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU) kwa lengo la kumuenzi mchezaji huyo aliyekuwa na mchango mkubwa kwenye Timu Taifa ya Gofu na TLGU kabla ya kufariki dunia.

Lina alikuwa ni miongoni mwa wachezaji waliopeperusha vema bendera ya Tanzania mwaka 2011, walipotwaa taji la Afrika Mashariki na Kati katika mashindano ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Dar es Salaam.

Makamu Rais wa TLGU, Ayne Magombe, alisema mashindano hayo yatafanyika katika mikoa tofauti na hiyo yote ni kuendelea kumuenzi mchezaji huyo kwa kuibua vipaji na kushindana, hivyo akawataka wachezaji kujitokeza kwa wingi ili kujishindia zawadi mbalimbali zitakazotolewa kwa washindi.

"Nategemea kuona ushiriki mkubwa wa wachezaji kama ilivyokuwa Moshi ambapo tulipata mwitikio mzuri, hiyo yote ni kuthamini kile ambacho alikifanya Lina enzi za uhai wake, alikuwa anapenda sana mchezo huu," alisema.

# AZIZ KI AMBWAGA CHAMA, FEI TOTO

**.Na Adam Fungamwango**

KIUNGO Mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara mwezi Machi, huku Kocha Mkuu wa Azam FC, Bruno Ferry naye akitwaa tuzo ya kocha bora wa ligi hiyo kwa mwezi huo.

Taarifa ilioyotolewa jana mchana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi Kuu, imesema kuwa washindi hao wamechaguliwa na Kamati ya Tuzo ambayo pia imemchagua Meneja wa Uwanja wa Lake Tanganyika uliopo Kigoma, Shaaban Rajab, kuwa meneja bora wa mwezi uliopita.

Aziz Ki, mchezaji wa Timu ya Taifa ya Burkina Faso, amewashinda viungo washambuliaji wenzake ambao ni Clatous Chama wa Simba, ambaye anaichezea Timu ya Taifa ya Zambia na Feisal Salum wa Azam, ambaye pia ni mchezaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

**Kamati imesema kwa Machi, Aziz Ki alionyesha kiwango kikubwa na kuisaidia timu yake kupata ushindi katika michezo mitatu kati ya minne ambayo timu yake imecheza, akifunga mabao matatu na kuhusika na mengine manne.**

Aliifunga Ihefu mabao 5-0, Geita Gold bao 1-0, Namungo mabao 3-1, lakini ikapoteza kwa Azam 2-1, Aziz Ki akicheza jumla ya dakika 330 katika michezo hiyo.

Kwa mujibu wa takwimu za Dawati la Nipashe, Aziz Ki, mbali na kuwa kinara wa kufunga mabao kwenye Ligi Kuu akiwa nayo 13 akiwa sawa na Fei Toto, ametoa pasi za usaidizi saba mpaka sasa, hivyo pia anaongoza kwa kuisaidia timu yake ya Yanga jumla ya mabao 20 hadi kufikia sasa.

Kwa upande wa Bruno, amewashinda Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi na Zuberi Katwila wa Mtibwa Sugar ambao aliingia nao fainali.




Rais wa Yanga, Hersi Said (kulia), akimkabidhi jezi ya timu hiyo, Balozi wa Tanzania Afrika Kusini, James Bwana, baada ya timu hiyo kuwasili mjini Pretoria nchini humo jana tayari kwa mechi ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundowns itakayopigwa katika Uwanja wa Loftus Versfeld, keshokutwa, Ijumaa. **PICHA: YANGA**

# Simba na 'jeshi' la watu 60 Misri

INATOKA UKURASA 24

Waziri huyo amesema serikali imewasiliana na mabalozi wa nchi za Misri na Afrika Kusini kuhakikisha timu zote mbili hazipati mkwamo wowote zinapokuwa huko.

"Kama ambavyo unafahamu, mpira una fitna nyingi, lakini nina wasiwasi tabia hizi zipo hasa upande wa huku Kaskazini ambako Simba inakwenda, huko wenyewe mnaita Uarabuni, huku ndiyo kuna tabu kidogo, huku Afrika Kusini hapana, Mamelodi Sundowns siyo Simba wala Yanga kwa Sauzi huko, kwa hiyo sitegemei kama huko watapata kashikashi, lakini ninachoweza kusema balozi zetu zilizopo katika nchi zote mbili zinafanya kazi kwa karibu sana na timu zetu hizi kuhakikisha hakuna mkwamo wowote ule, jicho la serikali liko macho, masikio yako wazi kuhakikisha kwamba hakuna linaloharibika kuelekea michezo hii ya marudiano," alisema.

Katika hatua nyingine, Kocha wa viungo wa zamani wa Klabu ya Simba, Zrane, amefariki dunia jana mchana nchini Rwanda ambako alikuwa akifanya kazi katika Klabu ya APR.

Taarifa zinasema kuwa kocha huyo alifariki dunia ghafla jana saa saba jijini Kigali, huku zingine zikisema kuwa alikutwa amefariki kwenye nyumba aliyokuwa akiishi jijini humo.

Klabu ya APR imethibitisha kifo cha kocha huyo raia wa Tunisia, ambaye mara ya mwisho alionekana katika mchezo wa Jumapili, Machi 31 dhidi ya Rwamagana City wa sare ya bao 1-1 akiwa mzima wa afya.

"Kwa masikitiko makubwa tunatangaza kifo cha kocha wetu wa viungo, Dr, Adel Zrane," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Akiwa nchini, Adel amewahi kuwa kocha wa viungo wa Simba kuanzia mwaka 2018 chini ya Kocha Patrick Aussems na kutimika 2021.

Akiwa Simba, alipata mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kushinda makombe matatu ya Ligi Kuu, mataji matatu ya Ngao ya Jamii, makombe mawili ya Azam Sports Federation Cup na Kombe moja la Simba Super Cup.

Mbali na mataji hayo alibaki kuwa kipenzi cha mashabiki na wanachama na klabu hiyo kutokana na kufanya kazi yake kwa bidii, akiwa na mapenzi makubwa na klabu, namna yake ya kushangilia pale timu inapopata bao, lakini pia kazi ya kuwaweka fiti wachezaji, ambapo hadi leo Wanasimba wengi wanaamini hajapatikana mtu sahihi kama yeye.

Klabu ya Simba imesema imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha aliyekuwa kocha wao wa viungo kilichotokea ghafla nchini Rwanda jana mchana.

"Zrane alikuwa mtu mkarimu, mcheshi na rafiki wa wachezaji na alipendwa na kila mmoja kipindi chote alichokuwa katika kikosi chetu tangu, 2018 hadi 2021," ilisema sehemu ya taarifa hiyo huku ikimalizika kwa kutoa pole kwa familia, Klabu ya APR, na wadau wote wa soka kwa msiba huo mzito.

Nipashe
# Michezo
Jumatano Aprili 3, 2024



**CRDB yadhamini FA Cup kwa bil. 3.7/-** UKURASA 20



Wachezaji wa Yanga wakiwasili Afrika Kusini jana tayari kwa mechi yao ya robo fainali Ligi Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundonws, itakayopigwa Uwanja wa Loftus Versfeld, Pretoria nchini humo keshokutwa, Ijumaa. **PICHA: YANGA**

# Pacome ampa mzuka Gamondi

## Asema sasa hana sababu ya kuihofia Mamelodi na anatarajia kupata...

**Na Saada Akida**

BAADA ya Pacome Zouzoua kurejea kikosini kwa kupona kwa asilimia 100, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameahidi kufanya mabadiliko makubwa katika kikosi chake kuelekea katika mechi ya marudiano ya robo fainali, Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundowns Ijumaa wiki hii.

**'Jeshi' lote la kikosi cha Yanga, akiwemo nyota huyo liliondoka nchini jana na kutua Afrika Kusini salama huku likipata mapokezi mazuri kutoka kwa Balozi wa Tanzania nchini humo, James Bwana.**

Katika mchezo huo wa mkondo wa pili utakaochezwa Uwanja wa Loftus Versfeld, Pretoria, Yanga inahitaji ushindi wowote ili kutinga nusu fainali baada ya mchezo wa kwanza Uwanja wa Benjamin Mkaba, Dar es Salaam kutoka suluhu.

Yanga iliwakosa Pacome, Khalid Aucho na Yao Attohoula katika mchezo huo wa kwanza kutokana na kuendelea kuuguza majeraha yao, lakini wachezaji hao wote wameongozana na timu na Gamondi ana uhakika zaidi wa kumtumia Pacome.

Akizungumza na Nipashe jana kabla ya timu hiyo kuondoka nchini, Gamondi alisema ana matumaini mkubwa ya kufanya vizuri katika mchezo huo wa marudiano dhidi ya Mamelodi Sundowns.

Alisema hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu mpinzani wake anafaida ya kucheza nyumbani lakini anaingia katika mchezo huo kwa kuziba njia zote ambazo wapinzani wao wanaweza kupata ushindi.

"Ni kweli Pacome amerejea kikosini na yupo fiti ninamatarajio makubwa ya kufanya mabadiliko ya kikosi katika mchezo wetu wa marudiano, wachezaji wanatakiwa kumwaga jasho ili kupata matokeo mazuri.

"Ukiwa na timu nzuri huwezi kuhofia mpinzani, malengo yetu makubwa ni kushinda mataji yote na kufanya vizuri zaidi, tunajua tunaenda kucheza na timu ya aina gani, licha ya kuzuia pia tunahitaji kushambulia," alisema Gamondi.

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba na 'jeshi' la watu 60 Misri

**Na Adam Fungamwango**

HUKU ikiwa katika majonzi ya kumpoteza aliyekuwa Kocha wao wa viungo, Adel Zrane, ambaye ametangulia mbele za haki jana nchini Rwanda, Klabu ya Simba imekwea pipa leo alfajiri kuelekea Misri tayari kwa mchezo wao wa marudiano wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaopigwa Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Kimataifa wa Cairo nchini humo.

Kwa mujibu wa Meneja Habari wa klabu hiyo, Ahmed Ally, walitarajia kuondoka na msafara wa watu 50 hadi 60 kwa ndege ya Shirika la Ndege la Misri na kwenda moja kwa moja hadi nchini humo ambapo leo jioni kikosi cha timu hiyo kitafanya mazoezi yake ya kwanza nchini humo.

Ahmed alisema katika msafara huo utakuwa na wachezaji 23, viongozi wa benchi la ufundi na viongozi wa Simba pamoja na mashabiki 17 ambao wamejilipia gharama zao wenyewe.

Alisema wanamatumaini makubwa ya kufanya vizuri katika mchezo huo kwa kuwa hata mechi iliyopita ambayo walipoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Al Ahly katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, walimiliki mpira na kucheza vizuri, lakini bahati tu haikuwa upande wao.

Wakati Simba ikieleza hayo, jana serikali kupitia kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma maarufu Mwana FA, alisema klabu hiyo nayo ilipiga hodi serikalini kuomba kupigwa jeki ya kupeleka mashabiki wake nchini Misri kwa ajili ya kuishangilia timu hiyo dhidi ya Al Ahly.


Akizungumza jana akiwa jijini Dodoma, Mwana FA, alisema serikali imepokea maombi ya Klabu ya Simba ya kupeleka mashabiki wake Misri kwa ajili ya kuiunga mkono timu hiyo kwenye mchezo huo wa mkondo wa pili, na maombi hayo yanashughulikiwa.

Hii imekuja siku moja tu baada ya serikali kuwasafirisha mashabiki 48 wa Yanga waliokwenda jijini Pretoria nchini Afrika Kusini kuishangilia timu hiyo itakapocheza mechi yake ya mkondo wa pili dhidi ya Mamelodi Sundowns, Ijumaa wiki hii, mchezo utakaopigwa Uwanja wa Loftus Versfeld, Pretoria.

"Jana (juzi) tumewaaga wapenzi 48 wa Yanga ambao walikuwa wanakwenda Afrika Kusini kwa basi, kushuhudia mchezo wa marudiano kati ya Mamelodi Sundowns na Yanga na baada ya jambo lile, Klabu ya Simba nayo imeleta maombi, ikumbukwe Klabu ya Yanga ilileta maombi mapema na tukafanya kama ambavyo tumelifanya, maombi ya Simba tunayashughulikia na naamini wapenzi wa Klabu ya Simba pia watapata nafasi ya kwenda kuhudhuria mechi kule Misri, kwa hiyo ni jambo tu la kiutaratibu, kwamba serikali inatakiwa kupewa taarifa kuwa klabu inahitaji nini na tuone kama iko ndani ya uwezo wetu kwa wakati huo na tunayafanya. Kwa hiyo nao Simba muda si mrefu watapewa utaratibu na klabu yao," alisema Naibu Waziri huyo.

Pamoja na hayo, Naibu

INAENDELEA UKURASA 23




Pumzika kwa amani Adel Zrane

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >